Burudani

## Ndoa ya Zuchu, Diamond 'gudubai'

Uk. 48



Tafakuri ya Askofu Bagonza

## Heri kuwa Zimbabwe kuliko kukimbilia Nigeria

Safu Uk. 10


# Pambazuko

Toleo Namba 173 Jumatatu, Julai 13-19, 2026


# Kitanzi muafaka Zanzibar


"Hatuwezi kutoa guarantee (uhakika) wa hilo. Kwa kweli hata sisi hatuna uhakika kama hiki kinachofanyika safari hii kitadumu kwa sababu kuna dynamics nyingi sana kwenye hizi siasa hasa katika mazingira ambayo tumeyapitia..."

Uk. 6&7

## Sababu Dangote kuchagua Kenya

SERIKALI ya Tanzania imetakiwa kutathmini mazingira yake ya uwekezaji baada ya kukosa fursa ya kujengwa kituo kikubwa cha kusafisha mafuta.

Uk. 22



## Jumuiya ya Madola yaikaba Tanzania

Uk. 12

## Hivi ndivyo Magufuli alivyopokonya pasipoti ya Askofu Niwemugizi

Uk. 14

## Sukari yenye mchanga yazua hofu

Uk. 20



## Tahariri

# Serikali itekeleze ahadi, isikilize sauti ya wananchi

SERIKALI ya Tanzania haina tena sababu ya kuendelea kulichelewesha suala la Katiba Mpya.

Kwa miaka mingi, Watanzania wamezungumza kwa sauti tofauti, lakini kwa ujumbe mmoja kwamba wanataka taifa lao liwe na mkataba mpya wa kijamii unaoakisi wakati uliopo, mahitaji ya kizazi cha sasa na ndoto za vizazi vijavyo.

Katiba siyo karatasi ya wanasiasa – kama alivyowahi kueleza mwanasiasa mmoja ndani ya Bunge Maalum.

Katiba ni roho ya taifa. Ndiyo dira inayopanga namna madaraka yanavyopatikana, yanavyotumika na yanavyodhibitiwa.

Ndiyo ngao ya haki za raia, uhuru wa taasisi, uwajibikaji wa viongozi na utulivu wa nchi.

Taifa linapokuwa na Katiba inayokubalika kwa mapana, hata ushindani wa kisiasa huwa na mipaka ya heshima, na wananchi hujenga imani kubwa kwa serikali yao.

Pambazuko tunaamini sasa ni wakati wa serikali kushtuka, kusoma alama za nyakati na kukumbatia matakwa ya wananchi wengi.

Swali la msingi siyo tena kama Tanzania inahitaji Katiba Mpya; swali ni lini na kwa utaratibu gani mchakato huo utakamilishwa kwa uwazi, ushirikishwaji na nia njema.

Jambo hili tayari lina baraka za kisiasa. Rais Samia Suluhu Hassan alipata kutamka kuwa katika kipindi chake cha uongozi atahakikisha Katiba Mpya inapatikana.

Kauli hiyo haikuwa ndogo hata kidogo, ilikuwa na inaendelea kuwa ahadi ya kiongozi mkuu wa nchi kwa wananchi wake.

Zaidi ya hapo, Chama Cha Mapinduzi (CCM), kupitia Ilani yake ya Uchaguzi ya Oktoba 2025, kiliahidi kufufua mchakato wa Katiba Mpya.

Hizi siyo kauli za pembeni; ni ahadi za kisiasa zinazopaswa kutafsiriwa kuwa hatua muafaka kwa sasa.

Kama serikali inaamini katika maridhiano, mageuzi na ustahamilivu, basi Katiba Mpya ndiyo uwanja mpana wa kuthibitisha imani hiyo.

Sisi Pambazuko tunaamini kuwa haiwezekani kuzungumza maridhiano bila kuandika upya misingi ya kuaminiana. Haiwezekani kuzungumza mageuzi huku tukiacha mjadala mkuu wa kitaifa ukiendelea kusukumwa mbele kama mzigo usiotakiwa. Aidha, serikali ikilifanyia kazi suala hili kwa utulivu na busara, itapunguza joto la malalamiko na kurejesha imani kwa wananchi.

Wapo wanaotaka tume huru zaidi, mgawanyo mzuri wa madaraka, haki imara za raia, uwajibikaji wa taasisi na mazingira bora ya ushiriki wa kisiasa. Haya siyo madai ya fujo; ni kiu ya kujenga taifa lenye misingi imara zaidi.

Tunashauri serikali itangaze kalenda rasmi ya mchakato huo. Ieleze lini mchakato huo wa Katiba utarejeshwa, lini maoni zaidi – kama yanahitajika yatahuishwa, lini rasimu itajadiliwa, na lini wananchi watapewa nafasi ya kuamua.

Ratiba ya wazi itawatuliza wananchi, itapunguza minong'ono, na itaonyesha kuwa serikali inachukulia ahadi zake kwa uzito.

Zaidi ya yote, mchakato huu usigeuzwe sherehe ya viongozi, bali uwe mjadala wa wananchi; vijijini, mijini, vyuoni, sokoni na kwenye vyombo vya habari.

Katiba Mpya haitakuwa ushindi wa chama fulani wala kushindwa kwa chama kingine, itakuwa ushindi wa Tanzania.

Itakuwa zawadi kwa vijana, wanawake, wafanyakazi, wakulima, wafanyabiashara, viongozi na hata wale ambao hawana sauti kubwa katika majukwaa ya siasa.

Kwa hiyo, Pambazuko tunasema; ahadi imekwishatolewa, matarajio yamekwishajengwa, na wananchi wanasubiri. Serikali isichelewe zaidi na kwa muda huu isigeuze nia kuwa mpango, mpango kuwa mchakato, na maelezo ya mchakato yanayofika mahali yanachosha kusikia.

# Mtoto akimpiga tafu mama yake...




*Mwanamke mwenye ulemavu akisukumwa na mwanaye kuvuka makutano ya barabara ya Mikocheni na Rose Garden jijini Dar es Salaam kama alivyokutwa na mpigapicha wetu jana.*

## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**


## TIMU YA PAMBAZUKO

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Mhariri Mkuu** | : | Simon **MKINA** | (simon@pambazuko.or.tz) |
| **Mhariri Mtendaji** | : | Peter **NYANJE** | 0784 211 716 |
| **Mwandishi Mkuu** | : | Elizabeth **HOMBO** | 0712 792 216 |
| **Mwandishi Mwandamizi** | : | Andrew **MSECHU** | 0769 415 815 |
| **Mkuu wa DTP** | : | Yassin **LUPATU** | 0782 009 971 |
| **Mkuu wa Utawala** | : | Tryruckia **MFINANGA** | 0744 768 263 |

*Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz*

Biashara

# IMF yaimarisha ushirikiano na serikali



*Balozi Khamis Mussa Omar akiwa na Zeine Zeidane. (Picha na WF)*

**Na Mwandishi WETU**

SERIKALI ya Tanzania imeimarisha ushirikiano wake wa muda mrefu na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), ikionyesha mwanzo wa hatua mpya ya ushirikiano unaolenga kuendeleza mageuzi ya uchumi.

Zaidi sana ushirikiano huo utaendelea kuiweka Tanzania katika ramani ya kufaidi ufadhili wa maendeleo na kuimarisha uthabiti wa uchumi wa taifa, kufuatia mazungumzo ya ngazi ya juu kati ya Waziri wa Fedha, Balozi Khamis Mussa Omar, na Mkurugenzi mpya wa Idara ya Afrika wa IMF, Zeine Zeidane.

Mazungumzo hayo yalifanyika pembezoni mwa Mikutano ya African Caucus 2026 inayofanyika jijini Banjul, Gambia, ambapo mawaziri wa fedha na magavana wa benki kuu kutoka nchi 54 za Afrika wanakutana na IMF na Benki ya Dunia kujadili vipaumbele vya maendeleo ya uchumi wa bara hilo.

Pande hizo mbili zilijadili namna ya kuimarisha zaidi ushirikiano wa kimkakati kati ya Tanzania na IMF, ambao kwa zaidi ya miongo sita umekuwa moja ya nguzo muhimu za maendeleo ya uchumi wa nchi.

Zeidane ameanza rasmi kuongoza Idara ya Afrika ya IMF akichukua nafasi ya Abebe Aemro Selassie, aliyemaliza muda wake baada ya kuwa mmoja wa viongozi waliotoa mchango mkubwa katika sera za uchumi za Afrika ndani ya taasisi hiyo.

Kwa Tanzania, mkutano huo ulikuwa fursa ya kueleza vipaumbele vipya vya maendeleo ya uchumi huku ukiimarisha ushirikiano na mojawapo ya taasisi muhimu zaidi za fedha duniani.

Ujumbe wa Tanzania ulijumuisha pia Waziri wa Fedha na Mipango wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dkt. Juma Malik Akil, pamoja na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Emmanuel Tutuba, jambo linalodhihirisha uzito ambao Serikali inaweka katika mahusiano yake na IMF.

Ushirikiano wa zaidi ya miaka 60

Ushirikiano wa Tanzania na IMF ulianza rasmi tarehe 10 Septemba 1962, mwaka mmoja tu baada ya kupata uhuru, wakati nchi ilipojiunga na taasisi hiyo.

Katika kipindi cha zaidi ya miaka 60 iliyopita, ushirikiano huo umebadilika kutoka msaada wa kawaida wa kusawazisha nakisi ya mizania ya malipo kwenda katika ushirikiano mpana unaojumuisha mikopo ya maendeleo, ushauri wa sera za uchumi, msaada wa kitaalamu na ujenzi wa uwezo wa taasisi.

Kwa mujibu wa Wizara ya Fedha, jumla ya ahadi za mikopo za IMF kwa Tanzania zimefikia Special Drawing Rights (SDR) bilioni 3.27, huku mikopo inayotekelezwa kwa sasa ikiwa na thamani ya takribani SDR bilioni 1.8.

Mbali na utoaji wa fedha, IMF imekuwa mshirika muhimu katika kusaidia mageuzi ya usimamizi wa fedha za umma, kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani, kuimarisha sera za fedha na kulinda uthabiti wa uchumi.

Taasisi hiyo pia imekuwa ikitoa msaada wa kiufundi kwa Benki Kuu ya Tanzania, Wizara ya Fedha na taasisi nyingine za umma ili kuimarisha utawala wa uchumi na utekelezaji wa sera mbalimbali.

Na Mzee TAI

# Tanzania isiendeshwe kwa hofu ya kila tangazo

KUNA wakati taifa linapaswa kusimama mbele ya kioo na kujitazama na kutafakari kwa kujiuliza; hivi kweli Tanzania imefika mahali inaogopeshwa na kila "Tom and Jerry?"

Kwamba kila tangazo moja la mitandaoni linaweza kufunga maduka, kusimamisha biashara, kukausha barabara na kufanya wananchi waamke asubuhi siyo kwa matumaini, bali kwa kuulizana, "leo hali ikoje?"

Hili siyo jambo dogo, ni kengele ya kutugutusha kwamba kuna mahali mambo hayajakaa sawa.

Katika siku hizi za Maonyesho ya 50 ya Sabasaba, Dar es Salaam, tumeona sura ya ajabu. Maonyesho ya biashara, ambayo kwa kawaida hutakiwa kuwa sherehe ya uchumi, ubunifu, wajasiriamali na fursa, yamefunikwa na kivuli cha hofu.

Wapo waliofunga biashara, walioshindwa kwenda kazini, wapo walioangalia barabara na kuona magari ya ulinzi, silaha za kivita na busara kuwaongoza kuwa siku hiyo ni kujifungia ndani.


Sasa tujiulize kwa uchungu mkubwa; kama wanaharakati wakitangaza jambo Saba Saba tunajifungia, wakitangaza Nane Nane tujifungie, wakitaja Oktoba 14 tujifungie, wakitaja Oktoba 29 tujifungie, wakitaja Desemba 9 tujifungie, na kesho wakitangaza jambo nayo tujifungie, tutafanya kazi lini, tutalima lini na tutauza lini?

Hapana. Nchi haiwezi kuendeshwa kwa kalenda ya hofu.

Serikali ina wajibu wa kulinda amani. Hilo halina mjadala, lakini kulinda amani siyo sawa na kuifanya jamii iishi kwa wasiwasi wa kudumu.

Miaka kadhaa iliyopita nakumbuka kwa umri wangu huu, siyo kwamba hakukuwa na matukio yenye kuleta hofu la hasha, bali vyombo vilifanya kazi zake kimya kimya na kwa weledi mkubwa, sasa sijui nini kimetokea.

Amani ya kweli siyo ukimya wa barabara tupu. Amani ya kweli ni pale wananchi wanapokwenda kazini bila kutazama nyuma, mfanyabiashara anapofungua duka bila kutetemeka, mama lishe anapowasha jiko lake bila kusubiri taarifa ya polisi, na kijana anapojadili siasa bila kuhisi kuwa maisha yake yako rehani.



Ifike mahali sasa serikali ipange kubadili mbinu za kuondosha hofu. Iwatumie viongozi wa jamii, dini, wafanyabiashara, vyama vya siasa, vyombo vya habari na asasi za kiraia kujenga ile Tanzania tuliyoizoea sisi na wengine wakati tunakua.

Ionyeshe nguvu ya hoja kabla ya kuonyesha nguvu ya bunduki, huku ikiwapa wananchi uhakika kuwa wanaweza kuendelea na maisha yao bila kuhofu maandamano, kamata-kamata au vurugu.

Wakati huohuo, wanaojiita wanaharakati nao wanapaswa kujitazama, haki ya kudai mabadiliko siyo tiketi ya kuharibu uchumi wa mtu mdogo.

Ukimfanya mama ntilie afunge biashara yake kwa hofu, hujamkomboa; umemuumiza. Ukimfanya dereva bajaji asifanye kazi, hujamjengea demokrasia; umemkata kipato.

Lakini mzigo mkubwa zaidi uko kwa serikali ambayo ndiyo yenye vyombo, mamlaka na wajibu wa kutuliza taifa, iende kazi kwa weledi na uaminifu mkubwa na nchi itakaa sawa.

Tanzania haiwezi kuendelea kuwa nchi inayotetemeshwa na kila ujumbe wa mtandaoni.

Wananchi wanahitaji uhakika, mazungumzo, kuamini kuwa nchi yao ni salama hata pale watu wanapoamka na kutanza kuwepo kwa hofu.

Ni wakati muafaka sasa serikali iondoe hofu kwa vitendo, isikilize, izungumze na ijenge imani ili kuondoa wasiwawasi kila uchao.

Naamini kuwa taifa linaloishi kwa hofu, hata likiwa kimya, halijatulia.

■ Habari Kuu

# Kitanzi muafaka Zanzibar



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi na Mwenyekiti wa Chama cha ACT Wazalendo Taifa, Othman Masoud Othman pamoja na marais wastaafu wa Zanzibar; Dkt. Ali Mohamed Shein, Amani Abeid Karume (katikati) wakishuhudia utiaji saini wa Tamko la Pamoja kati ya CCM na ACT Wazalendo kati ya Naibu Katibu Mkuu wa ACT Wazalendo - Zanzibar, Omary Ally Shehe na Naibu Katibu wa CCM - Zanzibar, Dkt. Mohammed Said Dimwa, Ikulu Zanzibar mwishoni mwa wiki. (Picha na Ikulu).*

**Na Mwandishi WETU, Zanzibar**

HATIMAYE mwanga umeanza kuonekana katika siasa za Zanzibar baada ya vyama hasimu visiwani humu; Chama Cha Mapinduzi (CCM) na ACT Wazalendo kukubaliana kuanza mazungumzo kuelekea kwenye muafaka wa kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Lakini katikati ya mwanga huo, Pambazuko limebaini kuwepo kwa mitego kadhaa ndani ya mchakato wa mazungumzo na pia katika hoja zilizowasilishwa kama ajenda za msingi wa mazungumzo hayo.

Mahojiano ambayo Pambazuko limefanya na viongozi wa juu wa vyama hivyo kwa nyakati tofauti pembezoni mwa hafla ya utiaji saini tamko la pamoja kuhusiana na mazungumzo hayo, yamebaini kuwa hakuna chama chenye uhakika kuwa muafaka utakaofikiwa wakati huu, utadumu.

Kila upande ulionekana kumtuhumu upande mwingine kuwa chanzo cha mtanziko wa kisiasa ambao huikumba Zanzibar kila baada ya uchaguzi na kuvurugika kwa makubaliano na muafaka ambao umekuwa kama ada kila baada ya uchaguzi visiwani humu.

Lilinukuu usemi wa mwanafalsafa mmoja aliyesema kuwa kufanya jambo hilohilo kila wakati huku ukitarajia matokeo tofauti ni wendawazimu, Pambazuko liliwataka vigogo hao kuuhakikishia umma kuwa kinachofanyika wakati huu siyo uwendawazimu.

Inaendelea Uk. 7



# Kitanzi muafaka...

Inatoka Uk. 6

"Hatuwezi kutoa guarantee (uhakika) wa hilo. Kwa kweli hata sisi hatuna uhakika kama hiki kinachofanyika safari hii kitadumu kwa sababu kuna dynamics nyingi sana kwenye hizi siasa hasa katika mazingira ambayo tumeyapitia…"

"Siyo kwamba hatuna imani na kinachofanyika, la hasha. Tuna imani sana na ndio maana tunashiriki, lakini kudumu au kutodumu kwa makubaliano siyo jambo la chama chetu peke yake," alisema mmoja wa viongozi wa juu wa ACT katika mahojiano na Pambazuko kwa sharti la kutotajwa jina lake kwa kuwa hivi sasa hayupo katika nafasi ya kusema kwa niaba ya chama kuhusiana na suala hili.

Kwa upande wake, Katibu wa Kamati Maalum ya NEC Zanzibar, Idara ya Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Khamis Mbeto Khamis, aliliambia Pambazuko kuwa chama chake hakipaswi kubebeshwa lawama zozote kuhusiana na yanayotokea Zanzibar kila baada ya uchaguzi.

"Tunazo sheria ambazo tumekubaliana tuzifuate. Sheria inaipa ZEC mamlaka ya kuratibu na kusimamia uchaguzi na ikitangaza matokeo yanapaswa kuheshimiwa, lakini kila mara wenzetu hawaheshimu hilo. Hivyo ni vigumu sana sisi kuweka guarantee ya jambo hili kwa sababu halisababishwi na sisi," alisema.

**Mitego ya muafaka**

Ukiacha kila chama kushindwa kutoa uhakikisho wa kudumu kwa makubaliano yatakayofikiwa safari hii, tamko ambalo vyama hivyo viwili vimelisaini lina mitego kadhaa ambayo inambana kila mmoja.

Jambo kubwa limo ndani ya hoja zilizomo kwenye tamko.

Baada ya kulipitia tamko hilo, Pambazuko imebaini kuwa limesheheni mambo ambayo kwa muda mrefu yamekuwa ni msingi wa malalamiko na madai ya ACT Wazalendo.

Mathalan, tamko hilo linaweka mkazo kwa pande zote kuhakikisha maslahi ya taifa ndio yanaongoza mchakato wa kutafuta muafaka wakati uzoefu unaonesha kuwa kila mwaka maslahi binafsi ya vyama na wanasiasa ndio yamekuwa yakivuruga makubaliano yaliyowahi kufikiwa huko nyuma.

Wachambuzi wa masuala ya kisiasa waliozungumza na Pambazuko nao wanahoji kuna nini ambalo litawalazimisha wahusika kuacha misimamo hiyo iliyodumu kwa zaidi ya miongo mitatu sasa.

Pia, kuna hoja ya kutunga sheria mahsusi itakayosimamia yale yote yatakayoafikiwa katika mazungumzo baina ya pande hizo mbili jambo ambalo linaiweka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mtegoni kwani sheria hiyo ikikiukwa basi yenyewe ndio itakuwa lawamani.

Kwa ujumla tamko hili linaonekana kubeba zaidi hoja za ACT Wazalendo ambazo iwapo zitakubaliwa, basi zinaweza kuanza kuleta mgawanyiko ndani ya CCM ambako mara zote wahafidhina wa Zanzibar wamekuwa wakionya kuhusu kuingia katika makubaliano ya kisiasa na mahasimu wao.

Wengi wanafikiria kuhusu muafaka wa kisiasa ambao utakiwezesha ACT Wazalendo kuingia kwenye serikali, lakini kwa mujibu wa mwenyekiti wa chama hicho, Othman Masoud Othman, huo ni mtazamo finyu wa kile ambacho chaka chake kinafikiria.


Kwa mujibu wa Othman, mtazamo sahihi wa kinachofanyika hivi sasa ni kuzaa Zanzibar itakayokuwa na hazina tano za utengamano wa kijamii; serikali yenye uadilifu, uwazi, utawala wa sheria na uwajibikaji; utulivu wa kisiasa na wa kiuamuzi pamoja na amani na utulivu endelevu.

Ili kuyafikia hayo unahitajika muda mrefu zaidi wa kujenga uaminifu baina ya pande zinazosigana, jambo ambalo linaweza lisifanikiwe katika muda mfupi ambao pande hizo mbili zimepeana kwa ajili ya mazungumzo.

Hata hivyo, Othman alisisitiza katika hotuba yake; "Juhudi za kujenga na kuipeleka mbele Zanzibar ili iweze kutimiza ndoto zake kwa faida na manufaa ya sasa na vizazi vijavyo, ni wajibu wetu viongozi wa ngazi zote za kisiasa,

Inaendelea Uk. 8

■ Habari Kuu




# Kitanzi muafaka...

Inatoka Uk. 7

kiserikali, sekta binafsi, na wa dini. Kulifahamu hilo na kuonesha njia sahihi kwa wananchi wote ni jambo la msingi sana."

**Makubaliano yalivyofikiwa**

Baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa mwaka jana, ACT Wazalendo ilisusia kujiunga katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) kama katiba inavyotaka wakidai kuwa walipokwa ushindi kwenye uchaguzi huo.

Hali hiyo ilileta sintofahamu visiwani humu kiasi kuwa baadhi ya viongozi wa juu wastaafu wakalazimika kuingilia katika kuleta upatabisho.

Inatajwa kuwa marais wastaafu wa Zanzibar; Abeid Aman Karume na Dkt. Ali Mohamed Shein ndio walikuwa mhimili wa kuzileta pande hizo pamoja ili kumaliza tofauti zao kupitia mazungumzo.

Mazungumzo hayo yalianza Novemba 9, mwaka jana baada ya Rais Dkt. Hussein Mwinyi kukubaliana na pendekezo la viongozi hao wastaafu.

Tangu wakati huo vikafanyika vikao kadhaa ambavyo vimezaa tamko la pamoja lililosainiwa wiki iliyopita katika viunga vya Ikulu ya Vuga Zanzibar.

Tamko hilo linatoa nafasi sasa kwa vyama hivyo kuanza mazungumzo ya hoja za msingi kuhusiana na matakwa ya kila upande na hadi kufikia mwishoni mwa mwezi ujao vinapaswa kuwa vimefikia muafaka utakaowezesha ACT Wazalendo kujiunga na SUK.

Baada ya hapo mchakato huo utafuatiwa na mazungumzo zaidi kupitia kamati maalum zitakazoteuliwa ili kuyaweka masuala yaliyokubaliwa katika muktadha wa kisheria, ili kutunga sheria ambazo zitahusika kusimamia makubaliano yatakayofikiwa.

Inaendelea Uk. 9

# Kitanzi muafaka...

Inatoka Uk. 8

“Na hili ni jambo muhimu sana kwa sababu kila mara tumekuwa tukikubaliana bila ya kuwa na msingi wa kisheria, hivyo mmoja anapokiuka makubaliano hakuna msingi wa kumwajibisha au hata kumwonesha tu kuwa amekosea…”

“Hatutaki kurudia kosa hilo,” alisema Ismail Jussa Ladhu, Makamu Mwenyekiti wa ACT Wazalendo upande wa Zanzibar.

**Tamko lenyewe**

Kupitia tamko hilo, vyama hivyo viwili hasimu visiwani humu vimetangaza rasmi kuanza awamu mpya ya maridhiano ya kisiasa.

Tamko hilo la pamoja linalenga kuimarisha umoja, amani, utulivu na mshikamano Zanzibar kufuatia uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, kwa mujibu wa Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ambaye pia ni Katibu wa Kamati ya Maridhiano, Mansura Mosi Kassim. Tamko hilo lilitiwa saini na vyama hivyo mbele ya Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais, Dkt. Emmanuel Nchimbi, Mwenyekiti wa ACT Wazalendo, Othman Masoud Othman, pamoja na marais wastaafu wa Zanziabar; Aman Abeid Karume na Dkt. Ali Mohammed Shein ambao wanatajwa kuwa ndio waliowezesha vyama hivyo kufikia hatua hiyo.

Tamko hilo linaeleza kuwa tangu kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992, karibu kila uchaguzi mkuu uliofanyika Zanzibar umekuwa ukigubikwa na migogoro na malalamiko yaliyoathiri hali ya kisiasa nchini.

Ingawa uchaguzi wa Oktoba 29, 2025 ulifanyika katika mazingira ya amani na utulivu, baadhi ya vyama vya siasa vilieleza kutoridhishwa na matokeo yake, jambo lililosababisha kutokuwepo kwa mwafaka katika uundaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kama inavyoelekezwa na Katiba ya Zanzibar.

Kutokana na hali hiyo, marais wastaafu wa Zanzibar, Dkt. Amani Abeid Karume na Dkt. Ali Mohammed Shein, waliwashauri viongozi wa CCM na ACT Wazalendo kuanza mazungumzo ya kutafuta suluhu ya kudumu.

Mazungumzo hayo yalifanyika chini ya usimamizi wao kupitia vikao tisa vilivyoanza Novemba 9, 2025 na kuhitimishwa Aprili 16, 2026, sambamba na kazi za kamati ndogo zilizowezesha kupatikana kwa ajenda muhimu za kushughulikiwa katika hatua inayofuata ya mchakato huo.

Katika tamko hilo, pande zote mbili zimekubaliana kuendeleza ushirikiano kwa lengo la kujenga maridhiano ya kudumu yatakayolinda amani, utulivu na mshikamano wa Zanzibar.

Aidha, zimeahidi kuchukua hatua za kuimarisha imani ya wananchi, wawekezaji na wadau wa uchumi kwa kuendeleza misingi ya utawala bora, demokrasia, uwajibikaji, utawala wa sheria na uchaguzi huru na wa haki.

Tamko hilo pia linaeleza kuwa mchakato wa maridhiano utakuwa shirikishi kwa kuwahusisha wananchi, vyama vya siasa, asasi za kiraia na makundi mbalimbali ya kijamii.

Viongozi wa pande zote wamekubaliana kuwa mazungumzo hayo yataongozwa na misingi ya ukweli, uadilifu na dhamira ya dhati, huku maslahi ya Zanzibar yakitangulizwa mbele ya maslahi ya kisiasa, vikundi au watu binafsi.

Kwa mujibu wa makubaliano hayo, tamko linaambatana na ajenda maalumu zitakazojadiliwa na Kamati ya Pamoja itakayoshauri mfumo na utaratibu wa utekelezaji wa makubaliano.

Chombo maalumu kitakachoundwa kwa mujibu wa sheria kitasimamia uratibu na utekelezaji wa hatua zote zitakazokubaliwa, huku utekelezaji wa mchakato huo ukianza mara moja baada ya kutangazwa kwa tamko hilo.

CCM na ACT Wazalendo vimemalizia kwa kutoa wito kwa wananchi wote wa Zanzibar kuunga mkono mchakato huo kwa kutoa ushirikiano wa dhati, wakisisitiza kuwa mafanikio ya maridhiano hayo yataimarisha utulivu wa kisiasa, mazingira ya uwekezaji, maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa Zanzibar pamoja na Tanzania kwa ujumla.

Tafakuri ya Bagonza



Na Dkt. Benson BAGONZA

# Heri kuwa Zimbabwe kuliko kukimbilia Nigeria

NCHI ya Zimbabwe, ikiongozwa na Rais Robert Mugabe ilijulikana kwa msimamo dhidi ya mabeberu na kusababisha mkwamo wa kiuchumi.

Mkwamo huo wa uchumi ulifanya maisha kuwa magumu zaidi kwa wananchi kiasi kwamba hata chakula kikageuka kuwa anasa.

Hata hivyo, Nigeria yenyewe imebeba taifa kubwa kwa kutambulika dunia nzima kuwa imejaa watu wenye kutapeli na kutamalaki kwa rushwa.

Huko Nigeria ni kawaida kabisa kuona polisi anamtoza rushwa polisi katika kituo kimoja.

Huko mambo haya ya rushwa ni kawaida kabisa na inaonekana wanaopaswa kuyakemea wameyabariki.




Sasa nawaza.

Sisi Tanzania kwa miaka mingi tulikuwa tunaigwa kwa mambo mengi mema na mazuri. Tukapokea wageni wa kujifunza katika kila sekta kutoka kila upande.

Hata hivyo, sasa kibao kimegeuka. Waliotuiga, tunaenda kujifunza kwao. Hii siyo kula pensheni kupitia watoto. Ni kuwanyonya watoto.

Hata tuliowakomboa na kuwaruhusu kutumia pasipoti na uraia wetu, sasa tunawazidi katika kutengeneza maudhui ya kuchekesha. Tunacheka, hawacheki.

Tulijitolea bila malipo kutoa taarifa za usalama wa taifa letu kwa uzalendo. Sasa uzalendo tumeuwekea bei.

Ninaambiwa kuwa kumeibuka biashara ya kuripoti. Kwamba ukiripoti ukweli unapata laki; ukimsingizia mtu laki tano. Hivi hakuna maskini mzalendo? Bajeti ikiisha tusiripoti?

Hii ni ajira mpya isiyohitaji usaili. Unaripoti, unapata laki. Uliyemripoti anampa laki mbili aliyepokea ripoti; kesi imeisha, wote tumepata. Tunagawana keki ya taifa.

Sina lengo la kuwachekesha au kuwaudhi. Yote mawili yanaweza kugeuzwa kuwa chanzo kipya cha kodi ya kucheka au kununa. Namaanisha kabisa. Hakuna bei ya uzalendo.

Hivi sasa ni kama taifa limevimba; kwenye vyama hakuko sawa. Polisi hawajalipwa posho, watawalipaje watoa taarifa.

Fikiri mpaka utoe jasho, tafuta maoni au rudi mezani mkayajenge na waandamanaji hewa.

Tukwepe kituko cha Mjaluo-kazi, "Kujifungua bila kuvua nguo za ndani."

***Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.***



Na Dkt. Hellen Kijo BISIMBA

Kona ya Dkt. Bisimba

# Somo kwa serikali raia kujifungia ndani

JULAI 7 inayotambulika kuwa Sabasaba ni siku yenye historia pana. Ni siku kilipozaliwa chama cha TANU, kilichosimama kidete kupambania ukombozi wa nchi kutoka kwa wakoloni.

Siku hii ilikuwa inaadhimishwa kwa muktadha huo, lakini baadaye ilibadilika na kuwa ni Siku ya Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam, ambapo mwaka huu ni miaka 50 tangu yaanzishwe.

Hivyo ukiangalia Sabasaba ina uzito kama siku kilipoanza chama cha ukombozi nchini na baadaye maonyesho haya maarufu sana.

Kama ilivyo ada, mwaka huu tulitarajia mvumo mkubwa sana wa kibiashara kupitia siku hii, lakini kinyume Jubilei hiyo ya miaka 50 haikuonekana.

Nimejiuliza hali iliyojitokeza siku hiyo imetupa somo gani kama taifa?

Badala ya kuwa siku ya biashara, maonyesho na watu kutoka kwenda kwenye uwanja wa maonyesho wa Mwalimu Julius Nyerere kwa hapa Dar-es-Salaam, tumeshuhudia siku hiyo watu wakibaki majumbani, mji ukikosa kabisa shamrashamra.

Badala yake mitaa ilipambwa na wingi wa polisi katika sare zao na bunduki mikononi huku helikopta ya doria ikipita.

Hapakuwa na amri rasmi iliyowakataza watu kutoka wala matangazo motomoto tuliyoyazoea kuhusu Sabasaba.

Tulitarajia sherehe za Sabasaba zitapambwa na viongozi kutoka nchi za nje, huku kiongozi wetu mkuu akiongea na wananchi kuhusu kukua kwa biashara yetu kimataifa.

Lakini kukawa kimya! Kwa hali hii ni muhimu kabisa kujitafakarisha kwamba kulikoni? Na tunaelekea wapi? Na kwa manufaa ya nani?

Ebu tutafute somo katika hali iliyojitokeza Dar lakini na karibu nchi yote.

Kwa siku hii moja watu kutotoka ni biashara ngapi zilidorora? Serikali ilipoteza mapato kiasi gani? Tazama jinsi hofu, tahadhari na hata kutokuamini hali ya usalama kulivyobadili maisha ya kila siku, hata baada ya kutolewa tangazo kuwa watu wasiwe na hofu.

Tukigeukia upande wa serikali ambayo kwa zaidi ya wiki ilionekana kujipanga na kuweka tahadhari kiasi cha kujaza askari polisi barabarani kwa kuhofia wananchi wake kujitokeza kuandamana.

Najiuliza tu, hivi nguvu zilizokuwa zikiandaliwa kukabili watakaotoka kuandamana zisingeweza kutumiwa kutoa ulinzi kwa watakaoamua kuandamana?

Niliangalia yaliyokuwa yanaendelea nikawakumbuka wajukuu zangu wanaopenda sana mchezo wanauita ‘hide and seek’ ambao siye tulikuwa tunauita mchezo wa kujificha.

Pamoja na kuwa askari walikuwa peupe waliokuwa wanatarajiwa inaonekana walikuwa wamejificha na wanasubiriwa tu wakijichomoza washughulikiwe.

Je, hii si ishara kuwa utulivu wa kweli haujengwi kwa uwepo mkubwa wa vyombo vya dola pekee, ilitakiwa wananchi waweze kuwa na imani kwamba kuna usalama ili wale waliokuwa hawana nia ya kuandamana wajue vipo vyombo vinatulinda tunaweza kuendelea na kazi zetu na kwenda kwenye maonyesho ya biashara tukijua tuko salama.

Uhuru wa watu wa kuendelea na shughuli zao haukuwepo na hata serikali haikuwahakikishia watu hilo zaidi ya kuwepo barabarani.

Uhusiano mzuri kati ya serikali na watu wake ni muhimu. Je, mazungumzo, uwazi na kuheshimiana pasipo kuviziana haiwezekani?

Hivi tunataka tujenge taifa ambalo watu wake wanatoka kwa kujiamini au taifa ambalo wananchi wanajifungia ndani kwa kuona hivyo ni salama zaidi?

Kipimo cha amani siyo utulivu wa mitaa iliyo tupu, bali ujasiri wa watu kuweza kuendelea na maisha yao wakiwa na imani na taasisi za kidola zinazowalinda.

*Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.*

Habari

# Jumuiya ya Madola yaikaba Tanzania



Na Mwandishi WETU

JUMUIYA ya Madola imetoa siku 30 kwa Serikali ya Tanzania kutafuta ufumbuzi wa sintofahamu za kisiasa na haki za binadamu.

Hatua hii – pamoja na mambo mengine, inabeba amri ambayo inaitaka Tanzania kumaliza kisheria ama vinginenvyo, kesi ya uhaini inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Antipas Lissu.

Kutokana na amri hiyo ya Lissu kuachiwa huru, jumuiya hiyo inaamini kuwa kesi hiyo ya uhaini inayomkabili Lissu ni ya kisiasa.

Lissu alikamatwa Aprili 9, 2025 na Jeshi la Polisi akiwa Mbinga, Ruvuma, muda mfupi baada ya kumaliza mkutano wa hadhara na baadaye kusafirishwa chini ya ulinzi hadi Dar es Salaam ambako alifunguliwa kesi ya uhaini.

Jumuiya ya Madola imetoa amri hiyo baada ya kupokea ripoti ya mjumbe wake maalum, Dkt. Lazarus Chakwera, Rais wa zamani wa Malawi, ambaye alizuru nchini kufuatilia mambo kadhaa ikiwamo mauaji yaliyotokana na vurugu wakati na baada ya uchaguzi mkuu wa 2025.

Dkt. Chakwera pia alichunguza sababu na athari za kuzimwa kwa mitandao ya kijamii, vikwazo dhidi ya watu wanaodai haki, kuminywa kwa uhuru wa kujieleza pamoja na kesi ya Lissu.

Katika ziara hiyo, Aprili 15, 2026, Dkt. Chakwera alikutana na Lissu akiwa gerezani Ukonga jijini Dar es Salaam.

Katika kikao hicho, Lissu alitoa masharti na mapendekezo saba yanayolenga kulinda demokrasia ikiwemo kuondoa kesi za uhaini dhidi yake ili kupisha maridhiano.

Dkt. Chakwera pia alitembelea mikoa kadhaa na kukutana na wadau wa siasa na masuala ya kijamii na uchumi.

Mwito huu wa Jumuiya ya Madola unamaanisha kuwa ripoti ambayo Dkt. Chakwera aliiwakilisha kwa waliomtuma, ilionyesha kuwepo kwa ukiukwaji wa haki za binadamu kwani mambo ambayo yametolewa na jumuiya hiyo ni malalamiko ya muda mrefu ya wanasiasa wa upinzani na wanaharakati hapa nchini.

Akizungumzia amri ya Jumuiya ya Madola kwa Tanzania, wakili wa kujitegemea, Peter Madeleka ameunga mkono akisema pamoja na kwamba Tanzania ni taifa huru, lakini pale inapoonekana inakiuka misingi ya haki za binadamu na utawala bora, jumuiya za kimataifa haziwezi kukaa kimya.

Amesema njia pekee ya Jumhuri ya Muungano wa Tanzania kuepuka matamko na amri kutoka jumuiya za kimataifa, ni kujiondoa kwenye jumuiya hizo na siyo vinginevyo.

"Suala la Lissu siyo tu kwamba serikali imekuwa ikipokea mwito wa kuachiliwa kwake kutoka jumuiya za kimataifa pekee, bali pia hata nchini jambo hilo limepigiwa kelele na wadau mbalimbali, hivyo ni muhimu serikali ikafanyia kazi," amesema Madeleka.

Serikali ilimshtaki Lissu kwa uhaini na kuchapisha taarifa za uongo mtandaoni, kwa madai kuwa kampeni ya "No Reforms, No Election" iliyokuwa inaendeshwa na Chadema, ilikuwa ikichochea uasi wa umma dhidi ya serikali.

Inaendelea Uk. 13

# Jumuiya ya Madola

Inatoka Uk. 12

Kampeni hiyo ililenga kudai mabadiliko ya sheria za uchaguzi ili kuhakikisha kuwa uchaguzi unafanyika katika mazingira huru na ya haki.

Katika kesi hiyo ambayo bado inaendelea Mahakama Kuu, Lissu anajiwakilisha mwenyewe baada ya kueleza mahakama kuwa mawakili wake walinyimwa fursa ya kuwasiliana naye kwa faragha na hivyo kuona vyema kujitetea.

Hata hivyo, serikali ya Tanzania imekuwa ikisisitiza kuwa kesi inayomkabili Lissu haijachochewa kisiasa na mahakama ipo huru katika kuisikiliza.

**Mengi zaidi yatakiwa**

Mbali na kutoa siku 30 za kuachiwa Lissu, mwito huo wa Jumuiya ya madola kwa Tanzania pia umeitaka serikali, ndani siku 60, kurejesha – kwa ukamilifu huduma za majukwaa ya kidigitali na kusitisha vitisho dhidi ya vyombo vya habari na watetezi wa uhuru wa kujieleza.

Pia, mwito huo umeitaka Tanzania, ndani ya siku 90, kuanzisha jukwaa la vyama vya kisiasa lisilopendelea upande wowote ili kuangazia mabadiliko ya mfumo wa uchaguzi, ushindani wa kisiasa, watu waliokamatwa na uwajibikaji.

"Tunaitaka Serikali ya Tanzania kuanzisha bila kuchelewa uchunguzi huru wa uhalifu uliofanyika kama ilivyopendekezwa na tume ya uchunguzi, ikiwemo masuala kama vile ulipaji fidia kwa waathiriwa," inasema sehemu ya ripoti hiyo.

Ripoti hiyo ilisisitiza pia kuwa itaitisha kikao kisicho cha kawaida Septemba mwaka huu, lakini kabla ya hapo Tanzania itapewa fursa ya kutoa ripoti kuhusu hatua ilizopiga kutekeleza mwito huo.




*Katibu Mkuu wa Chadema, John Mnyika (katikati) akizungumza na mwenyekiti wa baraza la wazee la chama hicho (Bazecha), Suzan Lyimo (kulia) na mwanasheria mkuu wa chama hicho, Dkt. Rugemeleza Nshala kabla ya kutangaza maazimio 15 ya Kamati Kuu kwa waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. (Picha na Pambazuko).*

Ana kwa Ana

# Hivi ndivyo Magufuli alivyopokonya pasipoti ya Askofu Niwemugizi

Na Mwandishi WETU

NI jambo la kustaajabisha, kushangaza na kuibua mjadala mkubwa kuwa uongozi, sheria, miiko, kanuni na maadili vinaweza kutupwa kando, badala yake nchi ikaongozwa kupitia matamko na matakwa ya mtu mwenye dhamana kubwa.

Kisa cha kupokonywa hati ya kusafiria (pasipoti) kwa Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Rulenge-Ngara, Dkt. Severine Niwemugizi, ni mfano halisi wa kiongozi wa nchi anavyoweza kutumia madaraka yake kukiuka kanuni, sheria na katiba. Ni vigumu kuamini, lakini ilitokea.

Kupitia mazungumzo maalum na Pambazuko, Askofu huyo kwenye makazi yake ya Uaskofu Ngara mjini, mkoani Kagera Juni 21, 2026, kiongozi huyo wa kiroho anasimulia namna Rais John Magufuli (sasa marehemu) alivyomuuliza endapo ni raia wa Tanzania, na siku chache baadaye hati yake ya kusafiria ilichukuliwa.

Anasema jambo hilo lilimtikisa, lakini halikumkatisha tamaa, aliendelea na kazi kama kawaida huku akiamini ipo siku litakwisha, na ndivyo ilivyotokea.

Askofu Dkt. Niwemugizi anasema baada ya mwaka mmoja kupita, alimweleza Rais Magufuli kwa uwazi namna ambavyo ameamua kumfanya awe mahabusu. Na baadaye Rais Magufuli mwenyewe alimpigia simu na kumweleza kuwa anamrudishia hati yake ya kusafiria.



"Ilikuwa kama utani. Tulikuwa kwenye maongezi ya kawaida na Rais Magufuli kwa simu, tulikuwa tunachati kupitia Whatsapp, akaniuliza wewe ni raia?

"Sikushtuka lolote, nilijua ni utani tu kwa sababu mtu aliyeniuliza swali hilo tunafahamiana miaka karibu 40 iliyopita, kumbe mwenzangu kwake haikuwa utani, alikuwa anamaanisha," anaanza kusimulia Askofu Dkt. Niwemugizi.

**Endelea na mahojiano…**

**Swali:** Serikali imewahi kukunyang'anya hati yako ya kusafiria, hii maana yake ni kwamba haki yako ya kuwa raia wa Tanzania ilitikiswa. Unazungumziaje tukio hilo?

**Jibu:** Ni kweli. Hati ilichukuliwa, nilikaa bila kusafiri kwa mwaka mzima na nilikosa matukio mbalimbali ambayo nilipaswa kwenda kuyafanya katika mwaka huo.

Ingawa sijawahi kulizungumza hili hadharani, kwanza ilikuwa kama utani, nilipoulizwa wewe ni raia wa Tanzania? Hata kama ninaulizwa na mamlaka zinazohusika, niliona kama utani.

Maana anayeniuliza huyu mimi nimezaliwa kabla yake, namfahamu kwa miaka kama 40. Lakini ndiye anayeniuliza wewe ni Mtanzania?

Kwa hiyo naweza kusema nilitikiswa kwa kuulizwa swali hilo, mimi nikijua nilizaliwa wapi, lakini baada ya muda siyo mrefu nilifahamu kwa nini imekuwa hivyo.

Inaendelea Uk. 15

# Hivi ndivyo Magufuli alivyopokonya...

Inatoka Uk. 14

Baada ya kufahamu hilo, nikasema basi, hili nalo litapita, lakini hatimaye nilimwambia mhusika (Rais Magufuli) kwamba, "wewe sasa unataka kunifanya niwe mahabusu."

**Swali:** Nani alihusika na suala hilo kwa ujumla?

**Jibu:** Ni Rais Magufuli mwenyewe, ilifika mahali ingawa sijui kama ni dhamira yake iliona kwamba hapa sio sawa. Yeye mwenyewe baadaye aliniambia hati yako utarudishiwa, na ikarudishwa, nikaendelea na kazi lakini basi kama ni kutikiswa nilitikiswa kwa namna hiyo.

**Swali:** Unafikiri sababu ya kunyang'anywa hati ilikuwa ni nini?

**Jibu:** Ilikuwa ni masuala tu ya kutofautiana kimtazamo, maana mimi nilitoa ushauri, ambao nilifikiri ni mzuri, kwa sababu wakati Magufuli alipoingia madarakani mwaka 2015 siku 100 za mwanzo alifanya kazi kubwa sana, akiwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Wakati wa maongezi yetu, nikampongeza nikawa nimemshauri, ndugu yangu ehee haya unayoyafanya ni mazuri sana, lakini ili yawe na ulinzi inabidi yawe na sheria nzuri ya kuyalinda ili yasiwe ya upepo wa msimu, siku wewe ukiondoka na yenyewe yanaondoka.

Kwa hiyo nikamwambia namna anavyopambana na ufisadi, maadili kazini, hayo yote unayoyafanya ungekuwa na sheria nzuri ambazo zinaanza na sheria mama yaani, katiba nzuri.

Nilimwambia ukiwa na Katiba nzuri, utafanya vizuri na utawabana wale unaowataka waenende kwenye maadili mema.

Nilimwambia Katiba tuliyonayo, sheria zilizopo hao wote unaowabana wakienda mahakamani watakushinda kwa kutumia sheria zilizopo, na utaendelea kuwalipa, badala ya kupunguza matumizi unayaongeza, na utaendelea kuajiri wengine huku ukiendelea kuwalipa waliokupeleka mahakamani.

Kwa hiyo nilimshauri nikamwambia hilo la Katiba mpya unaliweza kwa sababu msingi mzuri ulikuwepo, ile rasimu ya Jaji Joseph Warioba ilikuwepo, hususani yale masuala ya mwanzo ya maadili, sasa anzia hapo.

**Swali:** Ulipotoa ushauri huo alisemaje?

**Jibu:** Aliitikia akasema nimekuelewa, na akaongeza; ikifika wakati basi nitakutafuta tena. Nikajua sasa hili jambo limekwenda vizuri kumbe nisijue suala la Katiba haikuwa agenda yake.

Siku moja nikaalikwa na taasisi fulani ya kiraia walikuwa na mkutano wao wakaniomba nikawafungulie, walitaka kuanzisha mchakato wa Katiba wakaniomba nizungumze nao.

Nikasema sina cha kuzungumza isipokuwa ni hili ambalo hata mkuu nimeshamwambia, Katiba ikitengenezwa vizuri mambo yatakuwa mazuri, na atatuachia urithi mzuri sana.

Inaendelea Uk. 15



*Askofu wa Jimbo Katoliki, Dayosisi ya Rulenge Ngara, Severine Niwemugizi akiongoza ibada ya Misa Takatifu ya kumkumbuka na kumuombea Rais wa Awamu ya Tano, hayati John Pombe Magufuli. Machi 17, 2025.*

Ana kwa Ana

# Hivi ndivyo Magufuli

Inatoka Uk. 15

Hilo ndilo lilikuwa kosa, na likanigharimu, kwa hiyo shida ilianzia hapo, na nilipoielewa nikasema basi haya ni ya kupita.

**Swali:** Je umewahi kuhofia jambo lolote la kuhatarisha usalama wa maisha yako?

**Jibu:** Sijawahi kuhofia, hata niliponyang'anywa paspoti yangu, watu waliniuliza kama nina hofu yoyote. Nikasema mimi naamini kufa ni mara moja, kwamba ukifa ndiyo umeondoka, na Mungu alisema utapitia njia hiyo kuja kwangu, hivyo mimi sina hofu kwa kweli.

Siku zote ninataka kuwa na uhuru wangu. Mungu ameniumba na uhuru na mawazo yangu kama yatanigharimu, yanigharimu tu, lakini nayatoa kama ninavyoyahisi, na wala si kwa nia mbaya, kwa hiyo huwa sina hofu.

Mimi naamini mlinzi ni Mungu, kama igekuwa sio Mungu basi wale wanaomiliki vyombo vya dola wangekuwa hawafi, lakini hata kama wanalindwa, bado wanakufa.

Kwa hiyo kuhatarishiwa maisha, nasema Mungu ndiye mlinzi mkubwa kabisa, namtumaini yeye, nafanya kazi yake na ninajua ananilinda na akiruhusu niondoke, nitaondoka. Hiyo ndiyo imani yangu.

**Swali:** Je una lipi la kujivunia unapokaribia kustaafu?

**Jibu:** Cha kujivunia katika utumishi ni kumshukuru Mungu, alinipa heshima ya kuhudumu kama padri na kama askofu, maisha yangu aliyonipatia nimeyatumia katika kumfanya Mungu ajulikane na kutumikiwa na wote.



Ni vigumu kusema nimefaulu katika hili. Kutamba, hapana, Mungu amenitumia tu, kama ni mawazo, sipendi kusema nina cha kujivunia, ninajivunia utume alionipa, ilikuwa ndoto yangu tangu nilipomaliza elimu ya sekondari. Nilimuomba Mungu anipe kazi.

Akanipa kazi ya kuwa padri, nikaomba nihudumie watu wa pembezoni. Nimefundisha seminari kuu Segerea, kabla ya kuteuliwa kuongoza jimbo.

Nimebaki katika utumishi huu bila kukata tamaa, ingawa kuna mengi katika maisha yangu.

Nilipotimiza miaka 40 kama padri nilikwenda kuhiji Roma, na kusali pale kwenye kaburi la Mtakatifu Petro kwa kuniombea na kuwa kati ya warithi wa mitume katika umri huu. Kama kuna chochote kizuri wa kumshukuru ni Mwenyezi Mungu.

**Swali:** Kwa muda uliofanya kazi, ni jambo gani limewahi kukukera?

**Jibu:** Moja ambalo kwa kweli sitolisahau, ni mtu mmoja alinisingizia kwamba nimetumia maungamo yake kumwadhibu na kumwondoa katika utumishi, huku akijua kabisa hakuwa na imani; kwa sababu kuungama ni kitendo kitakatifu kabisa katika maisha ya mtu.

Sakramenti ya kitubio ni kitu kitakatifu kwa mujibu wa imani ya Kanisa Katoliki.

Ni afadhali ukatwe kichwa, lakini si kutoa siri ya maungamo. Sasa mtu akifika mahali akasema wewe umesikia maungamo yake, halafu ukamwadhibu; huyo anakutakia jambo baya kweli kweli. Katika sheria za kanisa wewe unatengwa na kwa kutoa siri ya maungamo.

Sasa hilo ni tukio moja ambalo sikulinyamazia, nilitaka kwenda mahakamani ili muhusika alithibitishe na mimi nimwambie mkubwa wangu kwa sababu ni kati ya kosa kubwa la jinai ya kiroho.

Lakini ilifika mahali ikawa ni uongo. Huyo mtu alikuwa anatafuta namna ya kujitetea kutokana na mwenendo wake.

Inaendelea Uk. 17

# Hivi ndivyo Magufuli

Inatoka Uk. 16

**Swali:** Ni jambo gani unaweza kulikumbuka na kujivunia kwenye utumishi wako?

**Jibu:** Katika utendaji sipendi mtu anayesema bila askofu hakuna kinachoweza kufanyika, kila mmoja ana nafasi yake. Nafasi ya askofu ipo sawa, lakini hilo halimaanishi bila yeye hakuna linaloweza kwenda. Hata wenzangu kwenye kazi huwa nawaambia.

**Swali:** Unazungumziaje huu utitiri wa maaskofu ulioibuka katika miaka ya karibuni. Je, hauathiri hadhi yenu?

**Jibu:** Sisi si wamiliki wa neno askofu, mtu yeyote anaweza kulala akaamka akasema yeye ni askofu, jamii kwa bahati mbaya inakutambua kadri unavyojitambulisha.

Wengine wanajitangaza ni maaskofu, mitume na manabii, kwa hiyo hatuna haki ya kuwazuia wasijiite hivyo, isipokuwa kama tunavyoambiwa kwamba askofu si jina la heshima, bali ni jina la utumishi, si heshima wala nafasi ya kipekee.

Swali ni je wewe ni mtumishi? Maandiko yanasema anayetaka kuwa wa kwanza atoe utumishi; ndivyo bwana alivyosema.

Mimi sihangaiki sana kusikia kila mmoja anajiita askofu, lakini nasema, je ninatoa huduma na utumishi wa kiaskofu kweli? Kwa maana ya kanisa husika?

Kwa sababu mwingine anajiita askofu ili apewe maslahi fulani, mimi siitwi askofu ili nipewe maslahi fulani. Lakini nitoe huduma fulani, ambayo kwa mujibu wa teolojia na mafundisho ya imani, askofu anapaswa kufanya huo utumishi. Sisi si wamiliki wa hivyo vyeo, isipokuwa mti utatambulika kwa matunda yake.

### Mrithi wake

**Swali:** Bila shaka unakaribia umri wa kustaafu; ungetamani mrithi wako aweje?

**Jibu:** Sisi tunasema Kanisa si mali ya mtu, ni mali ya Kristo, mtu yeyote anayepewa wajibu wa kuliongoza hili kanisa katika jimbo fulani sifa ya msingi kabisa anapaswa kuwa mchungaji mwenye upendo wa kichungaji.

Kama Bwana anavyosema; ‘mimi ndiye mchungaji, mchungaji anayetoa maisha yake kwa ajili ya kondoo. Kwa hiyo, huyo atakayekuja kuwa mrithi wangu ajijue yeye ni mchungaji.

Awe tayari kutoa maisha yake kwa ajili ya kondoo, mengine yatakuja kujazia. Kama ana maono asiyaonee wivu, kama ana maono ya kuleta jambo fulani ayatoe.

Maana yake ni Mungu amempa karama fulani azitumie kwa ajili ya maendeleo ya Kristo. Zaidi sifa kubwa ni upendo wa kichungaji, kwa ajili ya kondoo wa bwana waliowekwa chini ya uongozi wako.

### Ugumu wa jimbo

**Swali:** Baadhi ya majimbo ya Kanisa Katoliki huelezwa kuwa ni magumu kuyaongongoza, vipi kuhusu Rulenge- Ngara?

**Jibu:** Ugumu wa jimbo unaanza na viongozi, waamini hawana ugumu, isipokuwa mimi nikifika nikawa na tabia fulani.

Watu wanaweza kurudi nyuma, mengine yanatokana na malezi, mapokeo, mengine ni mahusiano ya mchungaji na kondoo wake. Waamini wa Rulenge-Ngara, wapo tayari kupokea mchungaji yeyote na kushirikiana naye.

Nikitolea mfano, huu mradi nilioanza nao wa kujenga Kanisa Kuu hapa Ngara Mjini, kwa mtazamo wangu nilidhani lingechukua miaka 20 kulijenga, lakini kazi inavyokwenda, tulikofikia kuna ushirikiano, mwitikio mkubwa; hata kama watu uchumi wao ni duni, lakini Mungu wao wanampenda, wanamtukuza vizuri.

### Wako tayari kugharamia.

Wana moyo wa kuchangia. Na wakiona michango, dhabihu wanazozitoa zinatumika vizuri watatoa hata kidogo walicho nacho.

Kwa hiyo ugumu wa waamini nafikiri unaweza ukawa wa kutengenezwa kutegemea unavyowaendea, unavyohusiana nao, unavyozungumza nao na kuona nina kiongozi au nina mtawala.

Inaendelea Uk. 18

## Ana kwa Ana



# Hivi ndivyo Magufuli

Inatoka Uk. 17

Mimi ninapowaomba kuchangia, nami ninakuwa wa kwanza kutoa mchango, kwa hiyo waamini wakiona askofu amekuwa wa kwanza, nao wanaona kwa nini wasitoe? Unaweza ukawa kwenye eneo lenye uchumi mkubwa sana, elimu kubwa sana lakini inategemeana unavyohusiana nao.

**Swali:** Nje ya utumishi wa neno la Mungu, unajishughulisha na nini?

**Jibu:** Nje ya utumishi najishughulisha na mambo ya ufugaji, kilimo, mashamba, hata kama sina utaalam mkubwa na muda mwingi, lakini hayo nayapenda.

**Swali:** Ratiba yako kwa siku ikoje?

**Jibu:** Nikiamka asubuhi jambo la kwanza ni kusali kumshukuru Mungu, baada ya hapo naingia kazi za kawaida, kama ni nje ya ofisi, ndani ya ofisi, na nikipata nafasi nafanya mazoezi kwa ajili ya afya; maana ukijali afya ya roho, lazima ujali naya mwili pia.

Tuna wajibu wa kutunza uhai aliotupatia mwenyezi Mungu, si vizuri kubweteka ukasema Mungu atafanya; kwa hiyo nikipata nafasi nafanya mazoezi ya kujenga mwili, baadaye nasali tena na kwenda kupumzika.

**Swali:** Unapendelea michezo ipi?

**Jibu:** Mimi napenda michezo lakini sichezi kutokana na umri. Zamani nikiwa sekondari niliwahi kucheza basketball, soka, volleyball ingawa sio kwa kiwango kikubwa.

Kwenye mpira mimi ni shabiki wa klabu ya Yanga. Naifuatilia kila inapocheza na isiposhinda nasikitika kidogo.

Kwa upande wa ulaya, nashabikia timu ya Real Madrid ya Hispania, Arsenal ya Uingereza na Borusia Dotmund ya Ujerumani.

**Swali:** Ni jambo gani unaweza kuwasihi Watanzania?

**Jibu:** Nawasihi sana tujenge umoja na mshikamano, tuache kubaguana kwa misingi yoyote inayoweza kutubagua. Sisi ni wamoja, ni taifa moja. Na hakuna anayeweza kuishi peke yake katika dunia hii.

Hakuna mtu anaweza kusema nchi hii tutaishi Wakristo tu, Wakatoliki tu, au dini nyingine.

Mungu ametuumba sisi wote tukiwa na tofauti za kiimani, tunaweza kusema huu ni utajiri wa kutuweka Pamoja.

Mungu wetu ni yule tunayemtafuta wote, tubaki na taifa moja kwa furaha na amani, tukitendeana kama watu tunaoheshimiana tukatendeana haki, tunaweza kuishi kwa amani na furaha.

Hii ni nyumba ya wote hakuna mwenye haki zaidi ya mwingine. Na viongozi wetu wasiwe chanzo cha kutugawa, watufanye tupendane, wasilete vitu vinavyotufanya tuumizane, tuvumiliane.

Jambo hili nilimwambia hata Rais Kikwete wakati fulani, na yeyote yule anayekuwa kiongozi wa taifa hili awawe chanzo cha kutufanya tupendane, lakini wakifanya yale ambayo yanatufanya kuchukiane, basi lawama zitakuwa juu yao.

### Historia fupi

Askofu Niwemugizi alizaliwa Kitongoji cha Kayanza, Kata ya Usavya Biharamulo. Akiwa na umri wa miaka mitano wazazi wake walihamia sehemu ya Muganza Lubanda Chato, na baada ya baba yake kufariki dunia mwaka 1963, walirudi tena Biharamulo na ndipo aliendelea na masomo katika sehemu mbalimbali ikiwamo Sekondari ya Nyakato mkoani Kagera.

# Uchumi wa bodaboda unaobeba gharama za jamii

Na Isaria MWENDE



USAFIRI na biashara ya bodaboda nchini Tanzania umekuwa ukipigiwa kelele kuwa moja ya sekta zilizoongeza ajira, lakini wapo watu wanaopinga hilo.

Katika muktadha wa uchumi, mjadala huu unakosa swali muhimu zaidi; je, mchango halisi wa sekta hii kwa taifa ni upi tukihesabu faida na gharama zake zote?

Hivi karibuni nimepata fursa ya kusoma moja ya ripoti ya mshauri wa biashara na mawasiliano ya kimkakati, inayodai kuwa sekta ya bodaboda huchangia zaidi ya Shilingi trilioni 31.68 kwa mwaka katika uchumi wa Tanzania.

Ripoti hiyo imewasilisha hoja kwamba bodaboda ni ajira kamili, imewawezesha vijana kujenga nyumba, kusomesha watoto na kuchangia uchumi wa taifa.

Kwa mtazamo wa haraka, hoja hizo zina mvuto. Hakuna ubishi kwamba maelfu ya vijana wanajipatia riziki kupitia bodaboda.

Ni usafiri unaorahisisha maisha ya wananchi na umefungua fursa nyingi za kiuchumi, lakini, baada ya kuisoma kwa makini, nilibaki na maswali mengi kuliko majibu.

Ripoti haielezi wazi ilipata wapi idadi ya bodaboda milioni 1.76 zinazodaiwa kutumika katika makadirio yake.

Haijaonyesha utafiti uliothibitisha kwamba kila mwendesha bodaboda hupata wastani wa Shilingi 50,000 kwa siku.

Haijaeleza ni waendesha bodaboda wangapi waliohojiwa, walichaguliwaje, wala utafiti ulifanyika katika maeneo gani ya nchi.

Hakuna maelezo ya mbinu ya utafiti, hakuna data inayoweza kuhakikiwa na hakuna uchambuzi wa kitaalamu unaoonyesha kiwango cha uhakika wa takwimu zilizotolewa.

Maswali haya siyo ya kubishana, ni maswali ya msingi ambayo kila ripoti ya kitaalamu ya utafiti inapaswa kuyajibu kikamilifu.

Hata kama tukikubali makadirio yote yaliyowasilishwa ndani ya ripoti hiyo, bado kuna upande mmoja ambao haukupewa uzito unaostahili.

Ripoti imehesabu mapato ya sekta, haijahesabu gharama zake, na hili ndilo eneo ambalo mjadala wa kitaifa unapaswa kuelekea.

Kanisani kwetu, tuna msharika kijana aliyepoteza mguu kutokana na ajali ya bodaboda, dereva wa bodaboda naye alijeruhiwa vibaya katika ajali hiyo.

Leo familia inachangishana fedha za kununua mguu bandia wenye gharama ya mamilioni ya shilingi.

Biashara aliyokuwa akiendesha ilisimama, hivyo kipato kimepotea na kuacha shida nyingi ikiwamo kukosekana kwa ada za Watoto sasa wanafamilia wamebeba jukumu la kumsaidia kwa muda usiojulikana.

Hiki siyo kisa cha kipekee, tembelea wodini katika hospitali zetu, zungumza na madaktari, wauguzi na wahudumu wa idara ya dharura, utabaini kwamba kuna madhila mengi kwenye biashara ya usafiri wa bodaboda.

Sikiliza simulizi za majeruhi na familia zao, utaanza kuona kwamba nyuma ya kila ajali kuna mlolongo mrefu wa madhara usioonekana wazi kwa wengi na haikugusiwa kwenye takwimu za mapato niliyosoma kwenye utafiti nilioutaja.

Inaendelea Uk. 32

Habari

# Sukari yenye mchanga yazua hofu

Na Mwandishi WETU

KARIBU miezi miwili sasa, watumiaji wa sukari wameshuhudia kuwemo kwa mchanga kwenye bidhaa hiyo.

Imebainika kuwa katika mzunguko wa bidhaa hiyo madukani wanunuzi na watumiaji wameibua malalamiko ya kuwemo mchanga na kuleta sintofahamu kuhusu ubora wake na hatima ya afya za walaji.

Uwepo wa sukari hiyo inayolalamikiwa kuwa na mchanga umeelezwa na watumiaji wa chai kuwa wamebaini kuwepo kwa mabaki ya mchanga kwenye vikombe mara wanapoitumia.

Pia, watumiaji wa bidhaa za ngano, ambao wamekuwa wakilalamikia mchanga katika mikate, keki, maandazi na bidhaa nyingine za ngano zinazotengenezwa kwa kutumia sukari hiyo.

Pambazuko limefanya uchunguzi kuhusu tatizo hilo, ambapo baadhi ya watengenezaji wa bidhaa hizo wamethibitisha kuwepo kwa sukari hiyo katika soko.

Wengi waliofikiwa na gazeti hili wameonya kuwa uwepo wa bidhaa sokoni kunadhihirisha kuyumba kwa vyombo vya udhibiti wa ubora, hivyo kuihatarisha maisha ya watumiaji.

## Malalamiko

Mmoja wa watengenezaji wa bidhaa za ngano aliyeko eneo la Tegeta (jina linahifadhiwa) alilieleza Pambazuko kuwa amekuwa akipata malalamiko kutoka kwa wateja kuhusu bidhaa zake ikiwemo mikate na maandazi kuwa na mchanga suala ambalo limekuwa likitatiza biashara yake.

Alisema ufuatiliaji walioufanya umebaini kuwa mchanga huo unaolalamikiwa unatokana na matumizi ya sukari kutoka nje ambayo ndiyo wanadhani ina mchanga.

Inaelezwa kuwa maduka mengi kwa sasa hayana sukari kutoka viwanda vya ndani.

"Kweli tumekuwa tukipata malalamiko ya mara kwa mara kutoka kwa wateja wetu, kwamba bidhaa zetu zina tatizo la kuwa na michanga..."

"Sisi uzalishaji wetu tunaufanya kwa kufuata viwango na kuzingatia kanuni zote za usafi, kwa hiyo ilitulazimu kutafuta chanzo cha tatizo hili..."

"Katika kufuatilia, tukabaini kuwa kuna aina ya sukari tunapoinunua lazima tatizo hilo lijitokeze, na hii inaonekana wazi kwamba ni sukari ya kutoka nje ambayo kwa sasa kwa karibu miezi mitatu ndiyo imekuwa ikipatikana kwa wingi madukani..."

"Baada ya kupata malalamiko hayo tumekuwa tukifuata bidhaa katika maduka tuliyopeleka na kweli tumejaribu kuzichukua na kuziloweka, mwisho wa siku tunakuta kuna mabaki ya mchanga fulani mwepesi sana yanajitokeza na kubaki chini," alisema.

Alieleza kuwa katika ufuatiliaji wao, walibaini kuwa sukari ya ndani kwa sasa inapatikana kwa nadra kutokana na wazalishaji kufunga viwanda kwa msimu, suala ambalo hufanyika kila mwaka kwa utaratibu wa viwanda hivyo kufanya ukarabati wa mitambo yao, wakati wakisubiri mavuno ya miwa.

Mmiliki wa duka la pamoja la bidhaa (Supermarket) liliyopo eneo la Makumbusho, Dar es Salaam alilieleza Pambazuko kuwa yeye pia amepata malalamiko kwa baadhi ya wateja kuhusu bidhaa za ngano ikiwemo mikate, keki na maandazi kuwa na mchanga, hasa katika kipindi cha miezi miwili iliyopita.

Alisema yeye amekuwa akitengeneza bidhaa zake ndani ya duka lake katika mazingira ya usafi na awali hakutambua chanzo cha malalamiko hayo kutoka kwa wateja, hadi alipofanya uchunguzi na kujiridhisha.

"Nilifanya ufuatiliaji wa kina na baadaye nikabaini kuwa tatizo linaanzia kwenye sukari. Kuna sukari hii ya nje ambayo ina rangi ya kahawia inaonekana kuwa ndiyo yenye shida, maana kila inapotumiwa lazima tupate malalamiko, lakini tukitumia sukari hii inayotengenezwa hapa ndani hatupati malalamiko..."

"Baada ya kugundua hivyo, tumechukua hatua ya kuwasilisha malalamiko yetu kwa wahusika ambao sisi tunajua ni TBS, japokuwa tumeambiwa kuwa hili linawahusu pia Bodi ya Sukari," alisema.

## Bodi ya Sukari

Pambazuko lilizungumza na mmoja wa maofisa wa Bodi ya Sukari ambaye alieleza kuwa yeye siyo msemaji, ila ni kweli kwamba wamepata malalamiko kuhusu uwepo wa sukari hiyo madukani na wanaendelea kufanya uchunguzi wao.

Inaendelea Uk. 21

# Sukari yenye mchanga

Inatoka Uk. 20

Pambazuko lilimtafuta Mkurugenzi wa Bodi ya Sukari, Prof. Kenneth Bengesi, na kumuuliza kuhusu malalamiko hayo, lakini akasema hawezi kuzungumzia suala hilo la kuwepo mchanga kwenye sukari kwa kuwa anayeshughulika na ubora wa sukari yupo na ndiye anayetakiwa kujibu hilo.

Alisema yeye anahusika na masuala ya utoaji wa vibali vya uingizaji wa sukari, uagizaji na uhakiki iwapo kiasi walichoagiza kimefika au la.

"Mimi suala ninaloweza kulizungumzia ni hasa iwapo vibali vimetolewa vingapi na ni akina nani waliopewa vibali hivyo, kiasi cha sukari tulichoagiza na iwapo kimeingia kwa wakati, kama hakijaingia na kama kuna uhaba wa sukari hayo ndiyo mambo ambayo ninaweza kuzungumzia..."

"Kimsingi, kuna wanaohusika na suala la ubora ndio wanaopaswa kuzungumzia suala hilo, kwa sababu ndio wanaofanya ukaguzi wa ubora wa sukari..."

"Wapo pia wanaohusika na kukagua masuala ya mionzi na mengine," alisema.

Alisema ni kweli kwamba bodi ndiyo inayotoa vibali vya uingizaji wa sukari nchini, lakini TBS ndiyo inayohusika zaidi na uhakiki wa ubora tangu kiwandani na hata inapoingia nchini.

Katika majukumu yake, Bodi ya Sukari nchini ndiyo inayohusika na kutoa, kufuta, au kusimamisha vibali na leseni kwa wazalishaji, wasambazaji, na wafanyabiashara wa sukari ili kudhibiti bei na kuzuia uuzaji holela.

Kwa mujibu wa taarifa ya Bodi ya Sukari, sukari inayozalishwa nchini mara nyingi hukosekana kwenye rafu za maduka kutokana na changamoto za msimu katika uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Pia, viwanda hufungwa kwa muda wakati wa shughuli za matengenezo ya viwandani, ambapo hufikia wakati viwanda husimamisha uzalishaji kwa muda, hivyo kulazimika kuagiza sukari kutoka nje, ili kuongeza nguvu kwenye akiba ya ndani.

Usimamizi huo hufanywa kupitia mfumo wa vibali vya dharura ili kuziba upungufu wa kibinadamu (nakisi) unaoweza kujitokeza, kama vile nyakati ambazo viwanda vya ndani hufanya matengenezo na kupunguza uzalishaji.

## Kauli ya TBS

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwango Tanzania (TBS), Dkt. Ashura Katunzi, alilieleza Pambazuko kuwa ni kweli wamepata taarifa ya kuwepo kwa sukari hiyo yenye mchanga kwenye mzunguko wa bidhaa hiyo na tayari walishachukua hatua za awali za ufuatiliaji. "Kama sehemu ya majukumu ya shirika na kwa kuzingatia misingi ya udhibiti ubora, shirika lilichukua hatua baada ya kupata taarifa ya malalamiko ya uwepo wa sukari iliyodaiwa kuwa na mchanga, ambapo ilifanya ukaguzi katika soko na kwenye maghala ya kuhifadhia sukari nchini..."

"Pia sisi hufanya uchunguzi wa kimaabara na kuweza kuzuia na kuondoa kwenye soko sukari iliyobainika kuwa na hitilafu," alieleza.

Hata hivyo, kiongozi huyo aligoma kuzitaja kampuni ambazo zimeingiza sukari hiyo.

Alisema shirika hutoa huduma kwa mujibu wa matakwa ya sheria, kanuni na viwango ambapo mojawapo matakwa hayo ni kutunza taarifa za wateja (confidentiality) kuendana na misingi ya udhibiti ubora na biashara duniani, kwa taasisi inayosimamia ithibati za umahiri za kimataifa.

Akaeleza kuwa bado wanaendelea kushughulika na kampuni hizo kiofisi.

Mkurugenzi huyo alisema TBS inaendelea kuimarisha udhibiti wa sukari inayozalishwa nchini na inayotoka nje ya nchi kupitia mifumo yake ya ukaguzi wa viwanda na maeneo ya uuzaji, uhifadhi na usambazaji, usajili wa maeneo ya uhifadhi, uthibitishaji ubora. Pia, akasema uchunguzi wa kimaabara, ukaguzi wa sukari inayoingia nchini na ufuatiliaji katika soko ili kuhakikisha kuwa bidhaa katika soko zinakidhi matakwa ya viwango na kuendelea kulinda afya ya walaji. Aidha, alisema TBS inaendelea kuhakikisha bidhaa za sukari zilizopo sokoni ni salama kwa matumizi, akiwataka wanaotilia shaka sukari kwenye soko,watoe taarifa kupitia simu ya bure namba 0800110827.

Hata hivyo, Pambazuko limeainisha kuwa jukumu kuu la TBS ni kulinda afya ya mlaji, usalama na mazingira kwa kusimamia na kudhibiti ubora wa bidhaa, kupitia utengenezaji wa viwango, upimaji wa bidhaa, ukaguzi, utoaji wa vyeti vya ubora, na usimamizi wa vipimo na mizani kote nchini. Hii ni pamoja na uanzishaji wa viwango kwa kuandaa, kuchapisha na kusambaza viwango vya kitaifa vya bidhaa na huduma, uthibitishaji wa ubora kwa kufanya vipimo na kutoa alama za ubora kwa wazalishaji.

Habari

# Sababu Dangote kuchagua Kenya



Aliko Dangote

Na Mwandishi WETU

SERIKALI ya Tanzania imetakiwa kutathmini mazingira yake ya uwekezaji baada ya kukosa fursa ya kujengwa kituo kikubwa cha kusafisha mafuta.

Kituo hicho kinachomilikiwa na tajiri nambari moja Afrika, Alhaj Aliko Dangote – wa Nigeria, sasa kinajengwa nchini Kenya.

Uamuzi wa Dangote umepoteza fursa adhimu kwa Tanzania endapo kituo hicho kingewekezwa Tanzania.

Wadau wameeleza kuwa uamuzi wa mfanyabiashara huyo mwenye ukwasi mkubwa, umetokana na masuala mengi ikiwamo utawala bora, usalama wa kibiashara, haki za binadamu na demokrasia.

Pia wameeleza kuwa Kenya, imetumia ujanja mkubwa kwa kuendesha kampeni ili Dangote awekeze kwao, huku wakitenga dola za Marekani milioni 65 ili kusaidia ujenzi huo.

Uamuzi huo wa Dangote kuchagua Kenya kwa ajili ya mradi huo mkubwa, umekuja miezi kadhaa baada ya Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Kenya, William Ruto, kujadili uwezekano wa Dangote kuwekeza katika mradi huo wa kusafisha mafuta Afrika Mashariki.

Vilevile Juni 28, 2026, Rais Samia alikutana na kufanya mazungumzo na Dangote kuhusu fursa mbalimbali za uwekezaji zinazolenga kuharakisha maendeleo ya uchumi wa Tanzania.

Hiyo ilikuwa ni mara ya pili kwa wawili hao kukutana katika kipindi kifupi.

Awali, walikutana Mei 16, 2026 na walijadili kuhusu uwekezaji wa ujenzi wa kituo cha kusafisha mafuta nchini.

Tanga ilikuwa miongoni mwa maeneo yaliyokuwa yakipewa nafasi kubwa kutokana na bandari na ukaribu wake wa mradi wa kimkakati wa bomba la mafuta ghafi kutoka Uganda, Eacop.

Katika hali iliyoshangaza wengi, akiwamo Rais Samia, katika mkutano mmoja wa kimataifa uliofanyika Nairobi, Rais Ruto alitangaza hadharani kuwa Dangote atashirikiana na nchi za Afrika Mashariki kuwekeza kituo kikubwa cha kusafisha mafuta ambapo kitajengwa Tanga.

Hiyo ilikuwa mara ya kwanza kabisa kwa taarifa hizo kuwekwa hadharani na kutolewa na Rais wa Kenya, katika mazingira yaliyoonekana kumshangaza Samia.

Wiki chache baadaye, Ruto alipokuja nchini Rais Samia akatumia nafasi hiyo kumkabili hadharani na kumtaka Ruto aeleze ni vipi alitangaza mipango hiyo wakati serikali ya Tanzania haikufahamishwa.

Baadaye Ruto aliporudi Kenya, serikali yake ilianzisha kampeni kubwa ya kuivutia Kampuni ya Dangote kuhamishia mradi huo Kenya.

Inaendelea Uk. 23

# Sababu Dangote

Inatoka Uk. 22

"Ruto alitumia ujanja na ndiyo maana aliporudi nchini kwake akaanzisha kampeni na serikali yake ikatenga dola za Marekani milioni 65 kwenye bajeti yake iliyoanza mwezi huu, hii yote ni kumvutia Dangote kwa lengo kusaidia ujenzi huo," amesema mchambuzi wa uchumi ambaye hakutaka kutajwa gazetini.

Rais Ruto amefanikiwa kucheza karata hiyo, ndiyo maana mfanyabiashara huyo mkubwa Afrika, sasa ametangaza rasmi kuwa atawekeza mradi huo nchini Kenya.

Tangazo la uamuzi huo imetolewa wiki iliyopita na Makamu Rais wa Dangote Industries anayesimamia mafuta na gesi, Devakumar Edwin.

Devakumar alitoa tangazo hilo wakati wa ziara ya ujumbe kutoka Kampuni ya Mafuta ya Jamhuri ya Demokrasia ya Congo katika kiwanda cha Dangote nchini Nigeria.

Baada ya tangazo hilo, mjadala mkubwa uliibuka huku wengi wakihoji kwa nini tajiri huyo namba moja Afrika ameichagua Kenya badala ya Tanzania?

**Wanazuoni wanena**

Mchambuzi wa uchumi, Profesa Samuel Wangwe amesema mfanyabiashara yeyote akitaka kuwekeza lazima aangalie mazingira mazuri zaidi.

"Unajua bado sijafuatilia, lakini ninachojua mipango yote ilikuwa inaenda Tanga, sasa kwa kuwa sijafuatilia naomba nisiongee sana, lakini ni wazi kwamba mfanyabiashara huwa anaangalia mazingira mazuri zaidi," amesema Profesa Wangwe.

Mhadhiri kutoka cha Chuo Kikuu cha SAUT-Mwanza, ambaye hakutaka jina lake litajwe gazetini, amesema mfanyabisahara huyo ameichagua Kenya kwa sababu nchi hiyo ina tofauti kubwa kati ya siasa na biashara.

"Huko Kenya wawekezaji hawazingatii amani na utulivu tu, bali pia na demokrasia, haki za binadamu na uhuru lakini ukiangalia hapa kwetu na yale yaliyotokea wakati wa uchaguzi uliopita, kuna tatizo kidogo na wawekezaji wanaogopa," amesema mchambuzi huyo.

Akitoa maoni yake, Mratibu wa Kitaifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa amesema mfanyabishara yeyote akitaka kuwekeza lazima aangalie mazingira ya kiutawala, kisiasa, uchumi na usalama wa biashara.

"Lakini jambo la pili ni masuala ya upatikanaji wa huduma za kuendesha biashara yoyote ile kama vile maji, barabara, umeme na vitu kama hivyo," amesema.

Olengurumwa amesema sababu nyingine ni suala la teknolojia lilivyo nchi husika, kwa sababu kwa sasa mambo mengi yanakwenda kwenye mifumo ya kiteknolojia.

"Pia jambo jingine kwa mwekezaji ni lazima aangalie wafanyakazi wenye ubora, weledi na viwango vikubwa vya elimu, lakini pia kuna masuala ya masoko, na vitu vingine visivyokuwa na shaka," amesema Olengurumwa.

**Sababu za Dangote**

Kampuni ya Dangote imeeleza kuwa sababu kubwa ya kuchagua Kenya ni kuuweka mradi huo karibu na Bandari ya Mombasa ambayo tayari ndiyo lango kuu la biashara Afrika Mashariki.

Sababu nyingine ni kutokana na mtandao mpana wa mabomba ya mafuta unaorahisisha usambazaji wa bidhaa kwenda Uganda, Rwanda, Sudan Kusini, Mashariki mwa DRC na hata sehemu za Tanzania.

Mradi huo ambao ni sehemu ya mkakati mkubwa wa Dangote wa kupanua biashara zake barani Afrika, ukikamilika itakuwa na uwezo wa kusafisha jumla ya mapipa 700,000 ya mafuta ghafi kwa siku.

Mradi huo utawapa Wakenya ajira 600,000 na bidhaa mbalimbali za petroli watazipata kwa gharama nafuu huku wakiendelea kujiimarisha kiuchumi.

Ujenzi wa kituo hicho unaotarajiwa kukamilika baada ya miezi 30, unakadiriwa kugharimu kati ya dola za Marekani bilioni 15 hadi 17 sawa na takribani Shilingi trilioni 2.2 za Kenya na Shilingi trilioni 46 za Tanzania.

Kilinge cha Mawasiliano



Na Loth MAKUZA

# PR isiyo ya kidigitali haionekani

WIKI chache zilizopita nilikutana na msimamizi mmoja wa mawasiliano wa kampuni fulani.

Aliniuliza swali ambalo nimekuwa nikitembea nalo kwa muda; "je, bado kuna afya yoyote katika njia ya zamani ya kufanya PR?"

Hakika hili ni swali zuri ambalo nami nilikuwa na jibu langu tayari mfukoni, tukakubaliana haraka kwamba bila kukumbatia digitali, basi PR huenda ikakwama.

Njia ya zamani haifi kwa sababu mtu ameiua, inafifia kwa sababu hadhira imehama nyumba na kusahau kuacha anwani mpya.

Kwa miaka mingi taaluma hii ilijipima kwa urefu wa habari magazetini, kwamba mteja anafurahi zaidi kuona bidhaa yake iko gazetini.

Hisia hiyo haikuwa mbaya ila sasa haitoshi. Kampuni inayopendwa na magazeti matata, lakini haionekani Google ni kampuni ambayo, kiuhalisia, haipo kwa mtu anayeitafuta saa tano usiku kwenye simu yake.

Hilo ndilo jambo gumu lililojificha nyuma ya msemo unaopendwa siku hizi; PR ya Kidijitali ("Digital PR") inaibadilisha tasnia."

Hakuna kilichosababisha mabadiliko haya kama tabia ya hadhira yenyewe kubadilika bila kuomba ruhusa. Vyombo vya habari vya kawaida bado vina thamani, lakini uaminifu usioweza kutafutwa ni uaminifu usioweza kuingiza faida.

PR ya kidijitali haikuja kufuta uhusiano wa vyombo vya habari, ilikuja kwa sababu njia ya zamani peke yake ilishindwa kujibu maswali ambayo watu wanayaandika kwenye kitufe cha kutafuta.

PR ya kidigitali imejenga daraja kati ya chumba cha habari na mtandao wa kijamii. Upande mmoja uhusiano na habari, upande mwingine uhandisi wa kuonekana - viungishi (backlinks) kutoka tovuti zenye uzito, maudhui yanayotambuliwa na akili mnemba, habari inayoendelea kufanya kazi hata gazeti likishafungwa.

Kwa ufupi, tasnia imehama kutoka kuwinda "kuchapishwa" kwenda kuhandisi "kuonekana." habari isiyopatikana ni habari ambayo, kiukweli, haikuwahi kusimuliwa.

## Vichwa vya habari kwenda viungo

Zamani mafanikio yalipimwa kwa unene wa faili la makala zilizokatwa magazetini, lakini leo faili hilo limebadilishwa na dashibodi isiyodanganya kama faili la zamani lilivyokuwa likidanganya mara nyingine.

Karibu asilimia tisini ya wataalamu wa PR wanasema viunganishi ndio matokeo yenye thamani zaidi.

Zaidi ya asilimia 75 wanatumia PR ya kidijitali kuinua uonekanaji na wageni tovuti. Karibu nusu ya kampeni zilizofanikiwa zinajengwa juu ya takwimu - utafiti, ripoti, namba ambayo hakuna mwingine aliyekuwa nayo.

## Ushirikiano ni silaha mpya

Jambo ambalo sikutegemea kuliona ni watu wa uboreshaji wa injini ya utafutaji (SEO) na watu wa Uhusiano na Umma (PR) wakikaa meza moja bila mmoja kumwangalia mwenzake kwa jicho la shaka.

Zaidi ya nusu ya wataalamu wa PR sasa wanafanya kazi bega kwa bega na wataalamu wa SEO na Akili Mnemba, wakikubaliana kwenye malengo ya pamoja.

Mchanganyiko huu wa ubunifu na takwimu ndio eneo ambalo PR ya kidijitali kweli inabadilisha tasnia: matokeo yanayopimika yakiwa na mguso wa moyoni.

## Ukweli mtupu

PR ya kidijitali haijaizika PR ya zamani, bali inafanya kile ambacho mwanafunzi mzuri hufanya kwa mwalimu wake; kuchukua mafunzo, kuhifadhi kinachofanya kazi, na kuifanya taaluma nzima kuwa kali zaidi mtandaoni.

***Mwandishi wa safu hii ni mtaalamu wa Uhusiano na Umma (PR). Anapatikana kwa namba: 0625 704 995 na kupitia email; projects@lothmakuza.co.tz***

Na Emmanuel JACOB



# Kwa nini vitisho havizuii unywaji pombe?



KWA miaka mingi kampeni nyingi za afya zimekuwa zikitumia jumbe mbalimbali kuonesha hatari ya unywaji wa pombe: “Acha pombe, ni mbaya kwa afya yako.”

Hata hivyo, wataalamu wa afya ya jamii sasa wanakubaliana kuwa ujumbe huu pekee hautoshi.

Watu wengi sasa tayari wanajua athari za pombe, lakini bado wanakunywa. Tunaona siri ya mabadiliko ya kweli haipo kwenye vitisho, bali kwenye kuelewa jinsi pombe inavyofanya kazi mwilini na jinsi tunavyoweza kubadili mifumo yetu ya maisha.

Kama wasomaji wangu kupitia gazeti la Pambazuko, ni wakati wa kuangalia suala hili kwa mtazamo mpya na jicho la kiuchambuzi.

Nini hutokea ndani ya mwili anapokunywa pombe? Badala ya onyo la jumla, ni muhimu kujua ukweli wa kibiolojia kwa mtu binafsi.

Pombe ina kemikali inayoitwa ethanol. Kemikali hii inajulikana kisayansi kama kichocheo cha saratani (carcinogen) ambacho huharibu mfumo wa vinasaba (DNA) vya binadamu.

Tafiti za hivi karibuni zinaonyesha kuwa unywaji wa pombe huongeza hatari ya kupata angalau aina saba za saratani, ikiwemo ya mfumo wa chakula, ini, na matiti, na inawezekana wengi hawajui.

Mtu anapojua angalau sayansi hii, unakuwa na uwezo wa kufanya uamuzi sahihi badala ya kufuata mkumbo.

Kwa sasa kuna mbinu kadhaa za kiusalama zinazoweza kupunguza madhara makubwa mwilini na kijamii ambazo ni kushushia na maji - Kunywa glasi moja ya maji baada ya kila glasi ya pombe ili kuzuia mwili kukauka maji (dehydration).

Kujipangia kipimo; kuwa na kikomo cha idadi ya vinywaji kabla ya kuanza na kwenda polepole.

Ulinzi barabarani; kuwa na dereva asiyekunywa (designated driver) au kutumia usafiri wa umma ili kuzuia ajali.

Watu wengi hutumia pombe kama njia mbadala ya kukimbia msongo wa mawazo au kupunguza machungu, hata hivyo, ukweli ni kwamba pombe huvuruga mfumo wa usingizi mzito (REM sleep) na huongeza viwango vya wasiwasi na sonona siku inayofuata.

Ili kupunguza hamu ya pombe, ni muhimu kutafuta njia mbadala za kukabili msongo wa mawazo, kama vile kufanya mazoezi ya mwili, au kushughulisha mwili, kazi za kijamii na ubunifu au maombi na ibada.

Ili kuwasaidia vijana kujiepusha na matumizi ya vileo, haitoshi tu kuwakataza, sote tunapaswa kutengeneza mazingira rafiki pamoja na nafasi za malezi, kuwekeza kwenye michezo na sanaa ambazo zitawapa burudani na faraja bila kuhitaji kileo.

Kubadili mtindo wa maisha siyo jepesi na halitokei kwa usiku mmoja, bali huanza kwa kupata uelewa sahihi na kuchukua hatua ndogo ndogo kuelekea maisha yenye afya na usalama zaidi.

***Mwandishi: Emmanuel Jacob, Ofisa Mfiziotherapia (Ameandika Kitabu cha Mbinu za Kutibu Maumivu Sugu). Simu: 0765359305 Instagram: Emmanuel Jacob***

Bustani ya Sheria



Na Karim Gabriel Mussa

# Bakwata siyo bodi ya usuluhishi wa ndoa



WATU wengi huamini kuwa kupeleka mgogoro wa ndoa Baraza la Waislam Tanzania (Bakwata) kunamaanisha tayari wametimiza matakwa ya sheria kuhusu usuluhishi wa ndoa.

Hata hivyo, Mahakama imeweka wazi kuwa Bakwata yenyewe siyo Bodi ya Usuluhishi wa Ndoa isipokuwa kama imeunda bodi hiyo kwa mujibu wa sheria.

Katika shauri la Shakila Ngoma dhidi ya Ally Katunga, lililoamuliwa na Mahakama ya Wilaya ya Morogoro Septemba 2, 2022, mahakama ilijadili uhalali wa usuluhishi uliofanyika Bakwata kabla ya shauri la ndoa kufikishwa mahakamani.

Wanandoa hao waliwasilisha Fomu Na. 3 wakidai kuwa tayari walikuwa wamepita katika usuluhishi uliofanyika Bakwata Wilaya ya Morogoro Mjini. Hata hivyo, mahakama ilichunguza iwapo kikao hicho kilifanywa na Bodi ya Usuluhishi wa Ndoa iliyoundwa na kutambuliwa kisheria.

Mahakama ilieleza kuwa Sheria ya Ndoa inataka migogoro mingi ya ndoa ipitie kwanza kwenye Bodi ya Usuluhishi wa Ndoa iliyoanzishwa kwa mujibu wa sheria.

Aidha, ilibainisha kuwa Katiba ya Bakwata haiifanyi taasisi hiyo yenyewe kuwa Bodi ya Usuluhishi wa Ndoa. Ingawa Bakwata inaweza kuanzisha bodi hizo, lakini lazima ziundwe kwa kufuata masharti ya sheria, zikiwa na mwenyekiti na wajumbe walioteuliwa rasmi.

Katika kesi hiyo, usuluhishi ulifanywa na Katibu wa Bakwata wa Wilaya ya Morogoro. Mahakama ilisema kuwa nafasi ya ukatibu pekee haimpi mtu mamlaka ya kuwa mjumbe wa Bodi ya Usuluhishi wa Ndoa bila uteuzi rasmi unaotambuliwa na sheria.

Vivyo hivyo, kuwa sheikh, mchungaji au askofu hakumfanyi mtu moja kwa moja kuwa mjumbe wa bodi hiyo.

Kutokana na kasoro hizo, mahakama ilifuta mwenendo wa usuluhishi uliofanyika Bakwata, ikafuta Fomu Na. 3 pamoja na hati ya talaka iliyotolewa kutokana na mchakato huo.

Pia iliwataka wahusika warejee kwenye Bodi ya Usuluhishi wa Ndoa iliyo halali kabla ya kufungua shauri jipya.

Uamuzi huu unatoa fundisho muhimu kwa umma kwamba siyo kila usuluhishi unaofanyika katika taasisi ya kidini unatambuliwa na sheria.

Kabla ya kufungua shauri la ndoa mahakamani, ni muhimu kuhakikisha kuwa usuluhishi umefanywa mbele ya Bodi ya Usuluhishi wa Ndoa yenye mamlaka ya kisheria. Kutofanya hivyo kunaweza kusababisha shauri kufutwa kwa sababu za kikanuni.

***Mwandishi ni Mwanasheria na Mchambuzi wa Sheria kutoka KGM Attorneys). Anapatikana kwa namba: 0755 395 572 au Email: karimbinmussa@gmail.com***



Na Rashid MTAGALUKA

# Muafaka sasa Zanzibar kuelewa somo

MIONGONI mwa hoja nyingi zilizotolewa na Mwenyekiti wa ACT Wazalendo, Othman Masoud Othman, wakati wa kusainiwa kwa tamko la pamoja kati ya chama chake na CCM wiki iliyopita, ni kuwa mchakato huo haukusudiwi kutatua mgogoro wa kisiasa pekee, bali kujenga taasisi imara, kurejesha imani ya wananchi na kuweka msingi wa maendeleo ya muda mrefu. Hiyo ndiyo hoja inayopaswa kujadiliwa zaidi.

Historia ya Zanzibar imeonyesha kuwa karibu kila uchaguzi mkuu umeacha majeraha ya kisiasa. Uchaguzi wa mwaka 1995 ulizua malalamiko makubwa, hali iliyoendelea mwaka 2000 na kusababisha matukio ya Januari 26-27, 2001 yaliyopoteza maisha ya watu kadhaa na kuharibu taswira ya Zanzibar mbele ya dunia.

Ndipo kukazaliwa Muafaka I na Muafaka II, ambapo ililengwa kurejesha maridhiano. Baadaye, kura ya maoni ya mwaka 2010 ikazaa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK), hatua iliyorejesha utulivu na kuifanya Zanzibar kuwa mfano wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya mazungumzo.

Lakini historia hiyo pia inafundisha jambo moja muhimu; makubaliano pekee hayatoshi. Kilichokosekana mara nyingi siyo utiaji saini wa nyaraka, bali utekelezaji wa yale yaliyokubaliwa.

Ndiyo maana kauli ya Othman kwamba sasa Zanzibar inapaswa kujenga taasisi zinazohakikisha haki, uchaguzi unaoaminika, utumishi wa umma usioegemea upande wowote na utawala bora, inapaswa kupewa uzito kuliko pongezi zilizotawala hafla hiyo.

Ikumbukwe kwamba, hakuna uchumi unaoweza kukua kwa kasi mahala popote pale duniani ikiwa mazingira ya kisiasa hayana utulivu. Zanzibar imejipambanua kama kitovu cha utalii, biashara na huduma katika Ukanda wa Afrika Mashariki.

Ni dhahiri kabisa kwamba, sekta hizo zinahitaji zaidi utulivu wa kisiasa, sheria zinazotabirika na taasisi zinazoheshimika.

Hivyo, mageuzi yanayozungumzwa leo siyo kwa manufaa ya wanasiasa pekee, bali ni sehemu ya mkakati wa kulinda ajira, kuvutia uwekezaji na kuongeza mapato ya wananchi.

Hata hivyo, wananchi wana sababu ya kuwa waangalifu. Othman mwenyewe alikiri kuwa wapo waliounga mkono mchakato huu, wapo waliokata tamaa kutokana na ahadi zilizowahi kutolewa bila kutekelezwa, na wapo wanaoupinga kabisa. Huo ni ukweli ambao haupaswi kufichwa. Imani ya wananchi haitajengwa kwa hotuba nzuri, bali kwa matokeo yanayoonekana katika maisha yao.

Sasa macho ya Wazanzibari hayapo tena kwenye tamko lililosainiwa, bali kwenye utekelezaji wake. Je, marekebisho ya mfumo wa uchaguzi yatafanyika? Je, taasisi za haki zitaimarishwa?

Je, utumishi wa umma utaendelea kuwa wa kitaaluma bila kuingiliwa na siasa? Maswali hayo ndiyo yatakayoamua kama safari hii Zanzibar imeamua kujifunza kutokana na historia yake au imefungua ukurasa mwingine wa ahadi ambazo hazitadumu.

Kwa mara nyingine, Zanzibar imechagua mazungumzo badala ya mivutano. Kilichobaki sasa ni kuthibitisha kwamba mazungumzo hayo yanaweza kuzaa mageuzi ya kweli.

Hapo ndipo wananchi watakapopata sababu ya kuamini kuwa historia inaweza kuwa mwalimu, badala ya kuwa hukumu inayojirudia kila baada ya uchaguzi.

***Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com***



## Habari

# Mvurugano vyama vya siasa




**Na Mwandishi wetu**

MWENENDO wa vyama vya siasa Tanzania unapita kwenye mtikisiko mkubwa baada ya viongozi wao "kutupiana" shutuma, huku vikao vya juu vya vyama hivyo vikiendelea kuwajibisha baadhi yao.

Ni dhahiri msemo wa waswahili unaweza kutumika, kuwa 'bundi" anaonekana kutua na kutulia katika baadhi ya vyama, ikiwemo Chaumma, Chadema, CUF na NLD, ambavyo kwa sasa vinapitia mchakato wa kile kinachotajwa kuwa "kusafisha viongozi wanaotuhumiwa kukiuka kanuni."

Pambazuko limebaini kuwa hatua hiyo ni mwendelezo wa yaliyotokea wakati na baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 29, 2025, hasa kutokana na matumizi ya fedha zilizopatikana kutoka serikalini kwa ajili ya kushiriki uchaguzi mkuu.

Aidha, vyama hivyo vimekuwa vikishutumiana kutokana na mapokeo ya baadhi ya viongozi kuhusu namna walivyopokea na kushughulikia vurugu za wakati na baada ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 29, 2025.

Kwa upande mwingine, viongozi wa vyama wamekuwa wakiendelea kukabana makoo kuhusu matumizi mabaya ya fedha na madaraka.

### CUF kwafukuta

Katika hali inayoonyesha kuwepo kwa kutoelewana na kufukuta kwa mgogoro ndani ya Chama cha Wananchi (CUF), tayari mmoja wa viongozi ambaye ni msemaji wa chama hicho ambaye pia ni mjumbe wa baraza kuu, mhandisi Mohamed Mshamu Ngulangwa ametangaza kujiuzulu nafasi zake.

Ngulangwa, katika barua yake kwa uongozi ambayo iliisambazwa pia kwa umma Jumamosi Juni 27, 2026, alieleza kuchukua uamuzi huo wa kujiuzulu nafasi ya ukurugenzi wa habari, uenezi na uhusiano kutokana na kile alichoeleza kuwa ni hatua ya kupata muda wa kukipambania chama hicho.

"Jumamosi Juni 27, 2026 nililazimika kusafiri kutoka Zanzibar kuja kuhudhuria kikao cha kamati ya mashauriano kwa upande wa Tanzania Bara, kilichoongozwa na Naibu Katibu Mkuu Bara, Vedasto Ngombale Mwiru.

"Pamoja na mambo mengine, kikao kiliona ipo haja ya chama kutoka hadharani kwa ajili ya kukemea tamko la Waziri wa Mambo ya Ndani, Patrobas Katambi, alipotoa zuio haramu kwa vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara,"alisema.

Alieleza kuwa kwa masikitiko, baada ya kutoa mwaliko kwa waandishi wa habari na wanachama kuhudhuria mkutano huo, mwenyekiti wake, Mirambo Yusuf aliagiza kusitishwa kwa mkutano huo kwa kile alichokieleza kwamba inaweza kumfanya aonekane hana maana.

Akizungumza na Pambazuko, Ngulangwa alisema tatizo linaloonekana ndani ya chama chake na vyama vingine vya siasa ni uwepo makundi mawili ya watu, moja likiwa na watu wanaoangalia namna ya kupambania na kufikia malengo ya vyama na jingine likiwa linapambania maslahi yao binafsi.

"Kuna watu wanaopigania na kuwaza kupata mabadiliko kupitia Katiba na sera ndani ya vyama, lakini kuna wengine wanaowaza namna ya kupata sabuni badala ya kutimiza malengo ya vyama, hapa ndipo tatizo linapoanzia," alisema.

### Chaumma wajipambanua

Katika kutafuta namna ya kujisimamia na kujirejesha katika misingi ya usimamizi wa malengo yao, Chama cha Ukombozi wa Umma (Chaumma) kimeingia katika mgogoro na kufikia hatua ya kumuondoa katika nafasi yake aliyekuwa katibu Mkuu, Salum Mwalimu na nafasi hiyo kushikwa na Benson Kigaila.

Inaendelea Uk. 29

# Mvurugano vyama

Inatoka Uk. 28

Uamuzi huu umefuatia taarifa za muda mrefu za kuwepo kwa mgogoro wa kiuongozi ndani ya chama hicho tangu kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29, 2025.

Jumanne, Julai 1, 2026 Halmashauri Kuu ya Chaumma ilihitimisha kwa kuweka wazi ukweli kuhusu kuwepo kwa mgogoro wa ndani ya chama hicho, ambapo mwenyekiti wa chama hicho, Hashim Rungwe alitangaza rasmi uamuzi wa kumvua madaraka Mwalimu kwa tuhuma za matumizi mabaya ya madaraka.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika kwa vikao vya juu vya chama hicho, Rungwe alisema Halmashauri Kuu iliamua kumwondoa Mwalimu kwa mujibu wa Katiba ya chama, na kwamba uamuzi huo umeanza kutekelezwa rasmi kuanzia Juni 30.

Mbali na madai ya kutumia vibaya madaraka, uongozi wa chama umemtuhumu Mwalimu kwa kukosa uwazi katika uendeshaji wa shughuli za chama, kubadili maamuzi ya vikao halali na kuyabadili kuwa misimamo yake binafsi.

Mwalimu alijiunga na Chaumma mwaka jana baada ya kujiondoa Chadema, ambako alikuwa Naibu Katibu Mkuu Zanzibar. Miezi michache baadaye alipitishwa kuwa mgombea urais wa Tanzania kupitia tiketi ya Chaumma, akisaidiana na mgombea mwenza Devotha Minja.

Wachambuzi wa siasa Tanzania wanasema mgogoro ndani ya Chaumma unaakisi changamoto za uongozi ambazo zimekuwa zikizikumba baadhi ya vyama vya upinzani.

Hatua ya kumwondoa inafuatia waraka uliowasilishwa Juni 29, 2026 na baadhi ya wajumbe wa Kamati Kuu na Sekretarieti ya chama, wakieleza kutokuwa na imani naye.

Wachambuzi wa siasa wanasema mgogoro huo unaakisi changamoto za uongozi ambazo zimekuwa zikizikumba baadhi ya vyama vya upinzani.

### Chadema hali tete

Wakati migogoro ikiendelea kufukuta katika vyama vya siasa, taarifa kutoka kwa baadhi ya vyanzo vilivyomo ndani ya Chadema zinaeleza kuwa hali ndani ya chama hicho si salama, kutokana na kufukuta kwa mvutano unaohusiana na matumizi mabaya ya madaraka na matumizi mabaya ya fedha, ukilenga kumwajibisha makamu mwenyekiti, John Heche.

Kwa mujibu wa vyanzo vya ndani ya chama hicho, katika mkutano wa Kamati Kuu ya chama hicho uliokaa mkoani Kigoma mwanzoni mwa wiki iliyopita, baadhi ya wajumbe waliibua tuhuma hizo dhidi ya Heche.

"Taarifa zinaeleza kuwa mjadala huo uliibuliwa bila woga na Godbless Lema ambapo aliiambia Kamati Kuu mbele ya Mwenyekiti kuwa amekuwa akichukua fedha kwa wadau bila kuzifikisha kwenye chama, Lema alitoa mfano wa Shilingi milioni 60 ambazo alimkutanisha mdau na makamu akazichukua na hakuna hata senti moja ambayo iliwasilishwa kwenye chama," kilieleza chanzo chetu kutoka ndani ya chama hicho.

Chanzo hicho kilieleza kuwa Lema alimtuhumu makamu mwenyekiti kwa kuwa mbinafsi ni kujitengenezea utukufu wakati Mwenyekiti wao, Tundu Lissu akiwa gerezani, ambapo ilieleza kuwa Heche alikubali kuvikwa uchifu alipokuwa Ruvuma.

Kilieleza kuwa mjumbe huyo alihoji kwamba Heche anakuwaje mfalme wakati Mwenyekiti wake akiwa jela? Na kwamba hiyo ni tamaa ya madaraka na ubinafsi, akisisitiza kuwa ndiyo maana hataki mwenyekiti atoke jela ili aendelee kuvaa ufalme na kupata michango kwa ajili ya familia yake.

Akizungumzia taarifa hizo, mkuu wa habari na mawasiliano wa Chadema, Gerva Lyenda alisema taarifa hizo si za kweli kwa kuwa vikao vilivyofanyika Kigoma vilikuwa na agenda mahususi.

"Ndugu yangu, hizo ni taarifa ambazo zinatungwa na kusambazwa mitandaoni na watu wasio na nia njema na chama chetu, hao ni maadui zetu. Vikao vyetu vimefanyika vizuri na tumefikia maazimio na makubaliano," alisema Lyenda.



Gerva Lyenda

## Barua za Wasomaji



**Tunakaribisha barua. Tuma kupitia**

**Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba; +255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz**

# Madereva fuateni sheria ya 'zebra'

**Mhariri,**
HAKUNA kitu kinatukera sisi watembelea kwa miguu tunapotaka kuvuka kwenye alama za kuvukia barabara (zebra crossing), tunajikuta tunakaa muda mrefu huku wenye magari yao wakipita kama hawatuoni.

Madereva wengi walivyo na roho mbaya, wakati mwingine unaweza kukuta mvua inanyesha au jua linawaka na wanakuona umesimama kwenye zebra lakini wala hawajali hadi atokee dereva anayefuata sheria na kujielewa.

Wakati mwingine ukiwa peke yako umesimama kwenye zebra ndiyo kipengele zaidi, utakaa muda mrefu hadi ujitangulize kidogo ndiyo magari yanasimama.

Madereva wenye tabia hii mjirekebishe, haipendezi kwanza inaonyesha kama mnatudharau sisi watembelea kwa miguu.

**Veronica Edmund**
**Mbezi Makonde, Dar**

# Hospitali za serikali zinakosaje huduma muhimu?

**Mhariri,**
HUWA ninajiuliza sipati majibu. Hivi ni kweli hospitali zetu za serikali zinakosa dawa, wauguzi na madaktari?

Nasema hivyo kwa sababu imekuwa ni jambo la kawaida kwenda kwenye hospitali za serikali kutibiwa na kuambiwa dawa zimeisha.

Tunashindwa kuelewa usimamizi ndiyo mbovu au tatizo ni nini hasa?

Sasa kama jiji kubwa kama la Dar es Salaam hospitali zake hazina madawa vipi kuhusu mikoani?

Mamlaka husika tunaomba jambo hili mlishughulikie kwa sababu linatia aibu taifa letu.

**Manka Dustan,**
**Tabata Mawenzi,**
**Dar es Salaam.**

# Watendaji wa vijiji wasitese wanafunzi

**Mhariri,**
NAOMBA nafasi nitoe kero inayowapata wanafunzi wa kidato cha sita ambao licha ya kufaulu masomo yao, wanakwamishwa na watendaji wa vijiji au mitaa katika kupata Namba za Mfumo wa Anuani za Makazi (NaPA) ili wazitumie kuomba mikopo.

Watendaji hao wamekuwa wakiwaomba wanafunzi hao Shilingi 10,000 wakidai ni za kununulia salio la vishikwambi wakati vitu vyote hivyo vinawezeshwa na serikali.

Mmoja wa watendaji wa mtaa wa ofisi yetu ya Kata ya Tambukareli, Wilaya ya Dodoma, (jina tunalihifadhi), amekuwa na visingizio hivyo ambapo wanafunzi wanaotoa wanahudumiwa haraka na wasiotoa wanaachwa wakati huduma hiyo ni bure.

Tunaiomba serikali, itoe tamko la kuwakemea watendaji wa vijiji na mitaa nchini ili wasiwakwamishe wanafunzi katika kuomba mikopo hiyo kwa wakati.

**Mwananchi kutoka Tambukareli,**
**Dodoma.**

# Mnyika ashambulia maridhiano

Na Mwandishi WETU

KATIBU Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), John Mnyika ameeleza kusikitishwa kwake na hatua ya chama cha ACT Wazalendo kuingia kwenye maridhiano na Chama Cha Mapinduzi (CCM akisema hatua hiyo ni sawa na kusaliti mapambano ya kudai Katiba Mpya.

Katika mazungumzo yake na wanahabari mwishoni mwa wiki, Mnyika alisema siyo kwamba chama chake hakiamini katika mazungumzo na maridhiano, bali hatua zinazochukuliwa kwa sasa zinaonesha kuwa hakuna nia ya kufikia maridhiano ya dhati.

Mnyika alisema amefuatilia kwa makini kutiwa saini kwa mchakato wa maridhiano kati ya ACT Wazalendo na CCM Zanzibar, Alhamisi Julai 9, 2026 na anaamini katika wakati muafaka chama chake kitalitolea kauli na msimamo.

"Sasa ninasema kwamba tutayazungumza haya na tutatoa mwelekeo, lakini ninachokiona ni kwamba kwa mara nyingine tena, pamoja na mauaji ya watu yaliyofanyika Oktoba 29, 2025 na siku zilizofuata, ACT Wazalendo imeamua kusaliti harakati za mabadiliko.

"Imezungumzwa kule kuwa moja ya mambo watakayozungumza watakapoingia kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa kupitia tume itakayoundwa ni kwamba watazungumza kuhusu mabadiliko ya katiba ya Zanzibar.

"Kwa matatizo yetu ya kikatiba zote mbili huwezi kushughulika na mapungufu ya katiba ya Zanzibar bila kushughulika kwanza na mapungufu ya katiba ya muungano..."

"Kwa hiyo kilichofanyika ni danganya toto ili Watanzania wajenge dhana kwamba sasa nchi ina maridhiano, kuonekane kuna maridhiano halafu upande wa pili umefungua mapambano, tunasisitiza tu kuwa msimamo wa kamati kuu ulishatolewa," alisema.

### Umuhimu wa maridhiano

Mnyika alisema chama chake siyo kwamba hakikubaliana na dhana halisi ya maridhaino katika mazingira yenye tija, lakini kutokana na hali iliyopo kwa sasa, kinasisitiza kuendelea na mapambano lakini kikiwa kimeacha wazi milango yake kwa mazungumzo ambayo yatakuwa ya haki.

"Tunaamini katika mapambano, tunaamini katika mazungumzo. Kuna mazungumzo ya dhati na tumesema tunataka mazungumzo ambayo yatakuwa na wasuluhishi huru hasa wa kimataifa, serikali inasema hatutaki mazungumzo, hatutaki wapatanishi, hatutaki wasuluhishi.

"Kwa hiyo kuna unafiki uliofanyika Zanzibar wa kusema kitu tofauti na kufanya tofauti, mimi nasema mazungumzo ni moja ya nyenzo ambayo sisi Chadema tunaiamini kama nyenzo ya kutatua matatizo," alisema.

Alisema kwa kufuatilia mwenendo wa mazungumzo ya Zanzibar kuanzia Novemba kati ya ACT Wazalendo na CCM kuna wapatanishi na wasuluhishi ambao ni marais wastaafu; Amani Karume na Ali Mohamed na msingi wa mazungumzo ya Zanzibar umejengwa kwa miaka mingi ambayo ulihusisha jamii ya kimataifa tangu Jumuiya ya Madola ilipokwenda kuingilia matatizo yao.

### Kuhusu kauli ya Rais

Mnyika alisema kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan kwenye utiaji saini wa tamko hilo huko Zanzibar kusema kwamba wanaharakati wanafanya ugaidi ni kauli hatari ikiachwa ilivyo na watetezi wote wa haki nchini.

Alieleza kuwa anayasema hayo kwa sababu kutokana na maandamano ya Julai 7, 2026 yaliyotangazwa huko mitandaoni, kuna viongozi wa Chadema ambao hadi hivi sasa bado wapo katika vituo vya polisi na wengine wameumizwa na kuteswa wakilazimishwa kuandika maelezo kwamba walipanga vitendo vya kigaidi.

"Wengine walilazimishwa kwa vipigo kutaja majina ya baadhi ya viongozi wa Chadema, sasa kutokana na matukio hayo kutokea siku chache kabla na hatua ya rais kutamka kuhusu wanaharakati na ugaidi, inatengeneza connection (muingiliano) kwamba kulikuwa na agizo," alisema.

"Leo wakati nchi inazungumza katiba mpya na free Tundu Lissu Rais anarudia kile kile, hii ni ishara kwamba hakuna maridhiano bali kuna tangazo la vita na viongozi wa Chadema," alieleza.

■ Biashara



# Uchumi wa bodaboda

Inatoka Uk. 19

Ajali moja inaweza kusababisha kifo, ulemavu wa kudumu, bili kubwa za hospitali, upotevu wa biashara, watoto kukosa ada, familia kuingia kwenye umaskini na ndugu kutumia akiba zao kumhudumia majeruhi.

Haya yote ni gharama za kiuchumi ambazo taifa hulipa, hata kama hazionekani kwenye jedwali la mapato.

Zaidi ya hayo, ukiukwaji wa sheria za usalama barabarani unaonekana wazi katika maeneo mengi ya nchi.

Ni jambo la kawaida kuona bodaboda wakibeba abiria wawili au watatu, bila kuvaa kofia ngumu, wakivuka taa nyekundu, kupita sehemu zisizoruhusiwa au kutumia hata njia za watembea kwa miguu.

Matokeo yake ni ongezeko la hofu kwa madereva wengine na watembea kwa miguu kutokana na mazingira yasiyotabirika barabarani. Bila kujua, taratibu wanasigina sheria za usalama Barabara kuwa mbaya.

Hali hii inavyoendelea itafika wakati sheria hizo za usalama barabarani hazitaonekana kuwa na maana yoyote.

Hili siyo suala la kulaumu waendesha bodaboda wote, wapo wengi wanaofanya kazi yao kwa uadilifu na kufuata sheria.

Tatizo ni kwamba ukiukwaji wa sheria unaofanywa na sehemu ya waendesha bodaboda umefikia kiwango kinachohitaji hatua za kisera na usimamizi madhubuti.

Serikali imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutumia sekta hii kupanua ajira kwa vijana. Hilo linapaswa kutambuliwa, lakini mafanikio hayo hayawezi kuwa sababu ya kupuuza changamoto zinazoongezeka kila siku.

Kinachohitajika sasa siyo mjadala wa kishabiki, bali utafiti wa kitaifa unaojitegemea. Utafiti huo unapaswa kupima mambo mawili kwa wakati mmoja.

Kwanza, mchango wa bodaboda katika uchumi kupitia ajira, mapato, kodi, biashara za vipuri, mafuta na huduma nyingine zinazotegemea sekta hiyo.

Pili, gharama zinazotokana na ajali, matibabu, ulemavu wa kudumu, upotevu wa uzalishaji, uharibifu wa mali, matumizi ya mifuko ya hifadhi ya jamii, bima na athari nyingine kwa familia na taifa.

Ni baada ya kufanya tathmini hiyo ndipo tutakapoweza kujua kama faida halisi ya sekta hii ni kubwa, ndogo au pengine imekaribiana na gharama zake.

Aidha, matokeo ya utafiti huo yanapaswa kuwa wazi kwa wananchi na pia kuwa msingi wa sera mpya kuhusu matumizi ya bodaboda nchini.

Serikali kwa mfano, inaweza kuzingatia mafunzo ya lazima kwa waendesha bodaboda, utoaji wa leseni unaohusisha mafunzo ya pekee ya usalama kwa bodaboda, usimamizi madhubuti wa sheria za barabarani, matumizi ya teknolojia katika usajili na utambuzi wa waendesha bodaboda, pamoja na uwekezaji katika miundombinu salama ya usafiri.

Bodaboda imekuwa sehemu muhimu ya mfumo wa usafiri wa Tanzania, hazitatoweka kesho. Haziwezi kuachwa ziendelee bila tathmini ya kina na usimamizi unaolingana na ukubwa wa mchango na athari zake.

Kwa hiyo, swali siyo kama bodaboda ni ajira au la, swali ni endapo taifa linafahamu gharama kamili na manufaa kamili ya sekta hii muhimu hasa kipindi hiki mafuta yalivyopanda bei.

Bila ushahidi wa kisayansi unaopima pande zote mbili za mizani, tutakuwa tunaendelea kujadili nusu ya tatizo huku nusu nyingine ikiendelea kugharimu maisha, afya na uchumi wa Watanzania kila siku.

***Mwandishi amejitambulisha kuwa ni msomaji wa gazeti la Pambazuko.***

# Tanzania yatajwa migogoro ya uwekezaji duniani

Na Mwandishi WETU

RIPOTI mpya ya Kituo cha Umoja wa Mataifa kuhusu Biashara na Maendeleo.

(UNCTAD - World Investment Report 2026) imeibua tahadhari kuhusu ongezeko la migogoro ya kimataifa kati ya wawekezaji wa kigeni na Serikali ya Tanzania.

UNCTAD inaitaja Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zilizofunguliwa mashauri mapya ya usuluhishi wa uwekezaji mwaka 2025.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, idadi ya mashauri yanayojulikana chini ya mfumo wa Investor-State Dispute Settlement (ISDS) imefikia 1,463 duniani kufikia mwisho wa mwaka 2025, baada ya kufunguliwa mashauri mapya 56 ndani ya mwaka huo.

Takribani asilimia 80 ya mashauri hayo mapya yaliwahusu nchi zinazoendelea, jambo linaloonyesha kuwa mataifa yanayovutia uwekezaji ndiyo yanayozidi kukabiliwa na migogoro ya kisheria inayohusisha wawekezaji wa kimataifa.

Ripoti ya UNCTAD inaitaja Tanzania pamoja na Angola, Bangladesh, Comoro, Guinea, Myanmar na Senegal kuwa miongoni mwa nchi zilizofunguliwa mashauri mapya ya uwekezaji mwaka 2025.

Hata hivyo, ripoti hiyo haielezi mwekezaji aliyefungua shauri dhidi ya Tanzania, sekta inayohusika wala kiwango cha fidia kinachodaiwa.

UNCTAD inabainisha kuwa hali hiyo inaakisi changamoto inayozikabili nchi nyingi zinazoendelea ambazo, pamoja na juhudi za kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDI), bado zinafungwa na mikataba ya zamani ya uwekezaji inayowapa wawekezaji haki pana za kufungua mashauri ya kimataifa dhidi ya serikali.

Ripoti inaeleza kuwa asilimia 85 ya mikataba ya uwekezaji inayotumika duniani ilisainiwa kabla ya mwaka 2010.

Mikataba hiyo imeendelea kuwa msingi wa mashauri mengi ya ISDS kutokana na vifungu vyake vinavyowapa wawekezaji ulinzi mpana, hali inayoweza kupunguza uwezo wa serikali kufanya maboresho ya sera bila kukabiliwa na madai ya fidia.

UNCTAD pia imebaini kuwa sekta ya madini na uchimbaji wa rasilimali iliendelea kuwa chanzo kikubwa cha migogoro hiyo.

Takribani theluthi moja ya mashauri yote mapya yaliyofunguliwa mwaka 2025 yalihusu shughuli za uchimbaji wa madini na rasilimali nyingine, huku mahitaji makubwa ya madini muhimu kwa mabadiliko ya nishati duniani yakiongeza migogoro katika sekta hiyo.

Kwa Tanzania, taarifa hiyo inaibuka wakati serikali inaendelea kutekeleza mkakati wa kuifanya nchi kuwa kitovu cha uwekezaji kupitia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (Dira 2050), inayosisitiza ukuaji unaoongozwa na sekta binafsi, uongezaji thamani wa madini, viwanda na miradi mikubwa ya kimkakati.

Wataalamu wa uwekezaji wanaeleza kuwa kadiri Tanzania inavyozidi kuvutia wawekezaji wakubwa, ndivyo umuhimu wa kuwa na mfumo madhubuti wa kisheria unavyoongezeka ili kulinda maslahi ya taifa bila kudhoofisha imani ya wawekezaji.

Kutokana na mwenendo huo, UNCTAD inapendekeza nchi kufanya mapitio ya mikataba yao ya zamani ya uwekezaji kwa kuweka masharti yanayolinda haki ya serikali kutunga sera za maendeleo, mazingira, afya na maslahi ya wananchi, huku ikiendelea kutoa ulinzi unaostahili kwa wawekezaji.

Ripoti hiyo inaonyesha kuwa zaidi ya nchi 80 tayari zimeanza kufanyia marekebisho mikataba yao ya uwekezaji ili kuendana na malengo ya maendeleo endelevu na kupunguza hatari ya mashauri ya gharama kubwa ya kimataifa.



■ Habari

# Vijana waliojenga Ikulu wapata mtetezi



Na Mwandishi WETU

VIJANA kadhaa waliotumiwa na serikali kujenga Ikulu ya Chamwino, Dodoma na kisha kudai kutelekezwa kwenye ajira, sasa wamepata mtetezi.

Mtetezi huyo ni Chama cha ACT Wazalendo kupitia katibu mkuu wa chama hicho na Mbunge wa Tunduru Kaskazini, Ado Shaibu Ado.

Akizungumza hivi karibuni, Ado amesema kuwa chama chake kitasimama kuwatetea vijana 436 waliokuwa wakitumikia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) walioshiriki ujenzi wa Ikulu mpya ya Dodoma ambao ni sehemu ya vijana walioahidiwa ajira jeshini, lakini baadaye wakatelekezwa.

Ado alisema hayo Jumatatu Julai 6, 2026 kwenye hafla ya kupokea wanachama wapya wa ACT Wazalendo kutoka vyuo vikuu vya Mkoa wa Dodoma iliyofanyika katika Hoteli ya Ulanga jijini Dodoma.

Mbunge huyo alisema vijana hao waliahidiwa ajira na Rais John Magufuli, kutokana na kazi ujenzi wa Ikulu ya Dodoma, lakini wengi wao bado hawatimiziwa ahadi hiyo.

"Wapo vijana wa jeshi la kujenga taifa waliopewa kazi ya kujenga Ikulu yetu hapa Dodoma wakati ule rais akiwa John Magufuli na walipewa waijenge kwa muda mfupi sana, vijana wale walifanya kazi usiku na mchana…"

"Rais Magufuli alipokwenda pale alishangaa hatua waliyoifikia na alitamka kuwa vijana wote zaidi ya 2000 watapewa kazi ndani ya jeshi kwa kazi nzuri mliyoifanya…"

"Leo hii ninapozungumza wapo vijana wa JKT wapatao 436 ambao baadhi yao wamepata changamoto za kiafya kwa kufanyishwa kazi za ujenzi wa Ikulu na ujenzi wa miradi mingine ya kimkakati, sasa wapo majumbani kwao…"

"Leo hao vijana wengi wakiwa wamepata changamoto ni kama wametelekezwa, wamerudishwa makwao, kwa lugha nyepesi maana yake wakajifie huko…"

"Ngome ya vijana ni kazi yenu kupaza sauti kwa sababu rais anaweza kuwaahidi watu na wasiipate hiyo nafasi, tunahitaji kuvunja huu utamaduni na tunauvunja kwa kusimamia ukweli," alisema.

Alisema ni rai yake kwa Waziri wa Ulinzi Dkt. Rhimo Nyansaho kufuatilia suala hilo na kuona uwezekano wa vijana hao kuajiriwa jeshini, kupewa ajira sehemu nyingine au kuwezeshwa mitaji ili wajiajiri.

"Ahadi ilitolewa vijana hawa 2000 wapate ajira jeshini, kama wana changamoto za kiafya walizozipata wakati wakitekeleza wajibu wao, watafutiwe ajira mbadala zinazowafaa na huyo ndio msimamo wa ACT Wazalendo…"

"Nitasimama hadi tone la mwisho la damu yangu kusimamia utekelezaji wa ahadi iliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa wakati ule wa awamu ya tano na inaendelea hadi sasa kwa sababu urais ni taasisi…"

"Natoa rai watafutwe walipo, tuzo wanayopaswa kupewa baada ya kupata changamoto za kiafya kwa kufanya kazi hiyo ni kuwachukua na kuwapa mazingira ya kufanya kazi na kama hawawezi jeshi wapelekwe kwenye kazi nyingine…"

"Kama haziwafai hizo wapewe mitaji ya shukrani kwa kazi waliyoifanya kwa kujenga ikulu," alisema.

**Kukazia kauli**

Kauli hiyo ya Ado ilikuwa ikikazia maagizo yaliyowahi kutolewa na Rais Magufuli, akitaka

Inaendelea Uk. 35

# Vijana waliojenga

Inatoka Uk. 34

vijana hao mara tu baada ya kumaliza ujenzi wa jengo la Ikulu wapelekwe jeshini na kuajiriwa kuwa askari katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

"Wakishamaliza hili jengo wapelekwe jeshini waajiriwe wawe wanajeshi, kwa hiyo mkimaliza katika kipindi cha miezi miwili, wakimaliza tu muanze kuandaa, hawa ninawapa ajira moja kwa moja. Walichokifanya ni kikubwa sana…"

"Ninajua na ninyi mliosimamia hii kazi mmesimamia kwa uadilifu mkubwa. Mmefanya kazi kubwa sana, mmetengeneza historia kwa nchi hii ya Tanzania, wapo watu wa nje waliotaka kuja kutujengea hii ikulu, huwezi ukajengewa makao makuu ya nchi na watu wa nje…"

"Ndiyo maana mimi ninawapopngeza ninyi ni mashujaa kama walivyo mashujaa wengine kwa sababu mmetumia nguvu zenu, busara zenu na zaidi kwa nishamu kubwa," alisema Magufuli wakati huo.

Magufuli alitoa ahadi hiyo Desemba 8, 2020, alipokuwa akizungumza na vijana 2,424 wa JKT pamoja na mafundi wa kiraia waliohusika katika mradi huo wa ujenzi, lengo lilikuwa ni kuwapa kipaumbele cha ajira ya kudumu jeshini kutokana na uzalendo, nidhamu na kazi kubwa waliyoifanya katika ujenzi wa Ikulu.

Hata hivyo, utekelezaji wa maagizo haya umekumbana na changamoto baada ya muda kupita, huku taarifa kutoka vyanzo mbalimbali na mijadala ya kisiasa ilieleza kuwa baadhi ya vijana hao waliripotiwa kuwa na changamoto za kiafya baada ya mradi wa Ikulu kukamilika.

**Vijana wazungumza**

Mmoja wa vijana hao ambao Pambazuko lilifanikiwa kumfikia (jina linahifadhiwa), alisema wamekuwa wakiishi katika mazingira magumu, ambapo tayari baadhi yao wamefariki kwa ajali wakiwa katika kijitafutia riziki zao.

Ameongeza kuwa wengine wamefariki kwa maradhi yanayotokana na athari za kazi waliyofanya na wengine wanaendelea kuugua wakiwa hawana msaada.

"Katika mawasiliano yetu, tumeshuhudia mwenzetu mmoja akifariki dunia kwa ajali, mwingine akifariki kwa maradhi ya kifua yaliyotokana na athari za saruji alipokuwa kwenye ujenzi na hakuwa na namna ya kupata tiba kutokana na ukata na mwingine amefariki dunia kwa maradhi na kukosa huduma," alisema.

Akaongeza; "Yupo mwingine aliyeko Dodoma ambaye kwa sasa tunavyozungumza anaugua, hana hata uwezo wa kugharamia matibabu yake na tunalazimika kumchangia kila mtu chochote alicho nacho."

Amesema kwa kuwa wengi miongoni mwao wanatoka katika familia masikini, kwa sasa wanaendelea kujihudumia kupitia vibarua maeneo mbalimbali na kazi za kuwawezaesha kikidhi mahitaji yao.

"Ukweli ni kwamba kwa sasa tunakumbana na mengi, kuna waliopata nafasi kwenye ofisi za watu, lakini baada ya kugusia kuwa walikuwa miongoni mwa walioshiriki kujenga Ikulu wanaanza kuogopwa, ni kwamba hatuko salama huku tulipo, watu wanatuchukulia tofauti kabisa," alisema.

Alieleza kuwa wamewahi kuandika barua Kwenda Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Rais-Ikulu kuomba serikali iwaangalie na iwape nafasi kwa kuwa wameshajengewa moyo wa uzalendo na wako tayari kuitumikia nchi.

"Sisi ombi letu kwa serikali na kwa Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye ana vyombo vingi vya ulinzi na usalama, atukumbuke, tuko tayari kulitumikia taifa kupitia huko…"

"Tunaomba atupe nafasi kwa vigezo vyetu kwa sababu wapo wenye elimu tofauti kuanzia shule ya msingi hadi wenye shahada, wapo waliokuwa wameingia kwa vipaji, mama anaweza kutuweka popote anapoona panafaa," alisema.

Kwa siku mbili mfululizo, Alhamisi Julai 9 na Ijumaa Julai 10, 2026 Pambazuko lilimtafuta Msemaji wa Serikali, Gerson Msigwa kupitia simu yake ya mkononi ili kupata kauli ya serikali kuhusu suala hilo, lakini muda wote simu yake iliita bila kupokelewa na hata alipotumiwa maswali kwa ujumbe mfupi wa maneno kupitia Whatsapp, hayakupata majibu.

Mtazamo

# Wanasiasa wasijimilikishe historia ya Tanzania


*Daraja la Kijazi Ubungo, Dar es Salaam*

Na Allan LAWA, Izazi

HISTORIA ya Tanzania kwa kiasi kikubwa imejazwa majina ya viongozi wa kisiasa na wenza wao, kana kwamba Watanzania wengine waliohudumu katika nyanja nyingine hawakuifanyia nchi yetu lolote.

Tembea nchini, kaskazini hadi kusini, mashariki hadi magharibi utaona majina ya wanasiasa wa miaka hiyo na wengi zaidi wa sasa ndiyo yanapamba majina ya mitaa, barabara, shule na maeneo maarufu karibu yote.

Ninaamini badaa ya kitambo kidogo tutaanza kuona majina ya watoto wa hao viongozi yakipamba pia maeneo kadhaa wa kadhaa nchini.

Ninasema haya siyo kwa kuwaonea gere wale ambao majina yao ndio yamekuwa utambulisho wa mitaa, madaraja, viwanja vya michezo, vituo vya mabasi, masoko makubwa au hata taasisi kama hospitali kwa kutaja vichache.

Baadhi ya viongozi majina yao yanatamba kwenye mikoa zaidi ya mmoja nchini ambako mitaa na taasisi nyingi nyingine zimepewa majina yao.

Historia ya nchi haiandikwi kwenye vitabu pekee, bali majina ya mitaa na taasisi nyingine ili kuonyesha nchi ilikotoka na waliohusika katika ujenzi wa nchi yao.

Hivi kweli, mke wa rais au mwenza wa kiongozi mkuu wa serikali jina lake inapewa taasisi wakati hana mchango wowote wa moja kwa moja wala siyo mwanataaluma wa hicho kilichopewa jina lake.

Sina wivu na walioolewa na viongozi wakuu wala jamaa zao kwani hata mie ningelikuwa na dada ningetamani aolewe na kigogo, nami nikaitwa shemeji wa rais, waziri au hata makamu wa rais na mtaa au kitu kingine kikapewa jina lake.

Tanzania, ukiwa mke wa mkubwa, ni sifa kubwa, inatosha kutunukiwa sehemu ya historia ya nchi yetu. Katika hili tumepotoka kama nchi. Turekebishe!

Sijaona mahali popote, wenza wa watawala wetu wa jadi kama, Mkwawa, Mangi, Mirambo, Mazengo kwa kutaja wachache, wamepewa heshima kwa mfano ya mitaa, shule isipokuwa hawa waliokuja baada ya uhuru.

Jambo baya zaidi hakuna anayeshughulika hata kujua majina ya wenza wa viongozi hao shupavu wa zamani na kuyaweka japo katika maandishi ya historia ya nchi yetu.

Nilitamani, kwa mfano mji wa serikali pale Dodoma, ungeitwa Mtemi Mazengo, mtawala wa mwisho wa wapwa zangu Wagogo, lakini unaitwa Magufuli City.

Hata hivyo, baada ya Magufuli kufariki, walioko serikalini wanalififisha jina lake kwa kupaita Mji wa Serikali Mtumba.

Ninajiuliza hivi kweli Dodoma iko mufilisi kwa majina ya mashujaa wa kukumbukwa, miongoni mwa Wagogo, au watani zangu Warangi au hata Wakaguru?

Mto Lumemo, pale Ifakara, uliokuwa korofi kwa miaka mingi, kumejengwa daraja kubwa na zuri, limepewa jina la aliyekuwa kiongozi wa awamu ya tano, Rais John Pombe Magufuli.

Inaendelea Uk. 37

# Wanasiasa wasijimilikishe...

Inatoka Uk. 36

Kwa Magufuli haijaishia hapo, bado amepewa daraja jingine refu zaidi Afrika Mashariki na Kati, palipokuwa kivuko cha Busisi mkoani Mwanza.

Ninajiuliza hivi kweli Wasukuma wangu hawa, watani wa Wahehe, nao kama Wagogo hawana mwingine katika kabila lao zaidi ya Magufuli anayepaswa kukumbukwa?

Hakuna Msukuma aliyekuwa hodari wa kupiga mbizi kuvusha watoto, akina mama na wazee waliokuwa wanatoka upande mmoja kwenda mwingine miaka hiyo? Kweli?

Huo ni mfano mmoja wa kiongozi mmoja ambaye pia mitaa kadhaa, baadhi ya taasisi nyingine kama vituo vikuu vya usafiri vimebeba majina yake. Viongozi 'wanajimilikisha' pekee yao historia ya nchi yetu. Hapana shaka nao wanapenda hivyo.

Mtwara, mji wa nguli wa soka nchini Mohamed Chuma, aliyechezea timu ya taifa kwa miaka mingi kuliko mwingine yeyote unayemfahamu hapa nchini, uwanja wao wa mpira unaitwa Nangwanda Sijaona. Nangwanda alikuwa mwasiasa wa miaka ya mwanzo wa uhuru wa Tanganyika.

Kwa mtazamo wangu, Nangwanda angelitafutiwa kitu kingine na uwanja huo ukapewa jina la Mohamed Chuma, mchezaji aliyelipigania taifa katika soka kwa miaka mingi hadi alipostaafu na kuagwa kwa heshima kubwa.

Hakuna mchezaji wa timu ya taifa ya soka hapa Tanzania aliyepata kuagwa kwa mchezo maalum kama yeye tangu Tanganyika kupata Uhuru mwaka 1961. Kama unamfahamu mwingine mtaje.

Ninasema tu. Siyo vibaya viongozi kupewa majina katika mambo kadhaa katika kutunza historia, kwani hata mie babu yangu Malinzanga ana kijiji kwa jina lake kwa heshima yake jimbo la Isimani, Iringa vijijini.

Kwa mfano wadi ya wazazi ya Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dar es Salaam ingependeza ikaitwa kwa jina la daktari wa kwanza kabisa katika Tanganyika huru wa magonjwa ya wanawake nchini, Dkt. Tito Andrew Mziray, maarufu Dkt. Andrew, kama ilivyo kwa wadi za Sewa Haji, Mwaisela na Kibasila.

Kama wapendekeza majina waliona haikuwa vema wadi ya wazazi kupewa jina la kiume, basi ingeitwa Esther Mwaikambo, profesa wa kwanza mwanamke bingwa wa magonja ya wanawake nchini.

Huko kwenye sekta ya michezo hali iko vivyo hivyo karibu viwanja vyote nchini, vinabeba majina ya viongozi wa siasa kama nilivyodokeza hapo juu kwa Nangwanda.

Uwanja wa Iringa unaitwa Samora Machel, Rais wa Kwanza wa Msumbiji, wa Tabora Ali Hassan Mwinyi na wa Mbeya; Sokoine kwa kutaja vichache.

Hata hivyo ule wa Songea, mkoani Ruvuma unaitwa Maji Maji, kumbukumbu ya vita vya kwanza kabisa vya ukombozi wa Tanganyika. Uwanja huu ulijengwa wakati mkuu wa mkoa alikuwa Lawrence Gama wa ukoo wa uchifu wa wangoni, naambiwa alikataa kuitwa Gama bali Maji Maji.

Hata hivyo, Rais Magufuli katika kipindi chake, pamoja na yeye kurundikiwa maeneo bado aliwagusa wahandisi wawili kwa kuwapatia madaraja ya juu (flyovers) makubwa kabisa nchini mawili katika kutambua michango yao.

Daraja la juu lililoko Ubungo Dar es salaam linaitwa kwa jina la aliyekuwa Katibu Mkuu kiongozi mhandisi John Kijazi.


Wakati aliyekuwa Mkurugenzi wa Tanroads, mhandisi Mfugale naye akaambulia daraja la juu lililoko eneo la Tazara jijini Dar Es Salaam.

Ninatamani wataalam wa fani zote watambuliwe kwa kupewa mitaa, miundombinu na taasisi walizozitumikia kwa ufanisi mkubwa katika kupanua historia ya nchi badala ya kuiweka kwa wanasiasa pekee kana kwamba nchi haijapata kuwa na watu wa taaluma nyingine waliochangia ujenzi wa Tanzania.

Tuanze kuandika historia jumuishi ya nchi yetu.

Ninasema tu.

## Wazo Binafsi




# Tusihadaike, tusimamie agenda ya Katiba Mpya

**Na Dkt. Ananilea NKYA**

IKIWA imetimia miezi kumi tu tangu ilipotokea mauaji ya raia wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29, 2025, hivi sasa kumezuka vuguvugu la kinachoitwa 'maridhiano' kwa lengo la kupooza moto wa kudai Katiba bora.

Kimsingi, kama Katiba bora haitapatikana mapema kabla ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2029 na Uchaguzi Mkuu 2030, kuna uwezekano mkubwa tunapokaribia uchaguzi, huenda tukashuhudia zaidi ya yale tuliyoyaona 2025.

Katiba bora ndiyo itawezesha kuundwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi ya kweli na siyo kwa jina lake tu, bali inayolindwa na kuongozwa na sheria bora za uchaguzi, vitu ambavyo vitafanya uchaguzi uwe huru na wa haki ili wananchi waweze kupiga kura kwa uhuru na haki, nchi ipate viongozi bora na siyo bora viongozi.

Tanzania kupata Katiba iliyoboreshwa ni muhimu sana kwa sababu Katiba ya sasa ya mwaka 1977, haikidhi mahitaji ya sasa ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Katiba hiyo imepitwa na wakati. Mathalan, wakati nchi ipo kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa, lakini Katiba, kwa kujua au kwa kutojua, ina vitu ambavyo vinaionyesha nchi kama iko kwenye mfumo wa chama kimoja cha siasa.

Kwa mfano Katiba ya (1977) imeweka mfumo dhaifu wa Muungano, inampa madaraka makubwa sana rais, imeweka mgawanyo dhaifu wa madaraka kwa vyombo vikuu vya utawala; Serikali, Bunge na Mahakama.

Pia Katiba mpya inatakiwa itupatie Tume Huru ya Uchaguzi ambayo itafanya kazi bila kuingiliwa na wananchi waone hivyo.

Kuwa na Tume yenye jina huru bila ya mifumo kuifanya ionekane kuwa huru, ni kiini macho.

Kwa hiyo, kutokana na udhaifu ilionao, Katiba ya sasa, katika nyakati hizi za mfumo wa vyama vingi vya siasa, haitaweza kutupa viongozi bora waliochaguliwa na wananchi kwa uhuru na haki ambao watawajibika kwa wananchi kikamilifu.

Uchaguzi huru na wa haki ni muhimu sana kwa sababu siyo tu utazuia maovu - mfano mauaji kutokea nyakati za uchaguzi, bali utatoa viongozi bora waliochaguliwa na wananchi ambao ndiyo wanakuwa rasilimali namba moja inayohitajika ili kuleta mabadiliko makubwa ya maendeleo ya nchi na wananchi wote.

Mfano nchini Singapore, Lee Kuan Yew, alipochaguliwa kuwa waziri mkuu alibadilisha kabisa maisha ya wananchi kutoka ufukara kuwa matajiri.

Aliweza kuboresha maisha ya wananchi kwa kiwango hicho kikubwa na nchi yake kuheshimika duniani kwa sababu baada ya kufanya mabadiliko makubwa katika mifumo ya uchumi, siasa na utamaduni ikiwa ni pamoja na utamaduni wa kuzuia kutoa na kupokea rushwa.

Kwa hiyo ni muhimu sana Watanganyika kuwa macho na kinachoitwa 'maridhiano' kitu ambacho kimeanza kupigiwa chapuo.

Inaendelea Uk. 39

# Tusihadaike...

Inatoka Uk. 38

Inaonekana watawala wanataka kupata kinachoitwa "maridhiano" na vyama vikubwa vya siasa vya ushindani (upinzani) hasa Chadema ili vihadaike, viache kudai Katiba bora kama walivyohadaiwa miaka mitano iliyopita.

Ninatoa hii tahadhari kwa sababu baadhi ya watu wanaosukuma kwenye mitandao ya kijamii dili la kinachoitwa "maridhiano" ni wanachama wa vyama vya siasa vya upinzani kikiwepo chama kikuu Chadema.

Mmoja wao nimemuuliza, je mbona siku za nyuma alikuwa anaendesha kampeni ya agenda ya wananchi; Katiba mpya, imekuwaje amebadilika ghafla na kuanza kusukuma agenda ya watawala?

Mtu huyo hakujibu swali langu, lakini mtu mwingine kwenye mtandao huo alinijibu akasema huyo jamaa ni njaa imembadilisha na kwamba huenda kuna kitu kapewa ametuliza njaa yake ndio anamtumikia aliyemlipa.

Ndiyo sababu tunawashauri wanachama na viongozi wa vyama vya siasa vya upinzani kwamba wawe makini, hata kama wana njaa ya tumboni, itabidi waweke maslahi ya umma mbele ili tusipoteze tena fursa ya nchi kupata Katiba bora kama tulivyopoteza miaka iliyopita.

Wajiulize maswali yakiwepo haya; Je, ni kwa nini watawala wanataka kutumia fedha za kodi za wananchi kufanya hicho kinachoitwa 'maridhiano' badala ya kuipa agenda ya Katiba bora kipaumbele ili hali wanajua kwamba chanzo cha kukosekana amani ya kweli nchini kwa sasa ni mauaji ya Oktoba 2025.

Je, ni kwa nini watawala wanataka maridhiano na vyama vya siasa wakati nchi ni ya wananchi wote ambao kama Katiba bora itaandikwa umma wote utapata amani na furaha ambavyo ndiyo maridhiano halisi?

Je, kama kinachoitwa 'maridhiano' siyo mradi wa kuhadaa umma na kupoteza muda Katiba isiandikwe, ni kwa nini wakati huu viongozi wa chama kikuu cha upinzani walioamua kusimamia agenda ya Katiba mpya wanapigwa vita?

Itoshe kutahadharisha kwamba wananchi wote, na wanachama wote wa vyama vyote vya upinzani msipokuwa macho kuepuka kudanganyika kwa fedha, vyeo, kutupiana tuhuma za mchongo au chochote kile hakika Katiba Mpya haitapatikana.

Tukumbuke, watawala wetu hawana utashi wa kisiasa kuhusu kuandikwa Katiba bora, hivyo ili wakubali, kunahitajika msukumo mkubwa sana na endelevu kutoka kwa wananchi, mwananasiasa mmoja mmoja, vyama vyote vya siasa vya upinzani na mashirika ya kijamii wakiwepo viongozi wa dini zote.

Inakaribia miaka 40 sasa wananchi tumekuwa tukidai Katiba bora, lakini haijapatikana kwa sababu agenda hiyo wamekuwa wakiachiwa watawala na vyama vya siasa vya upinzani.

Kwa hiyo, kuanzia sasa, wananchi wote, taasisi za kiraia zikiwepo za dini na na vyama vyote vya upinzani tuisimamie agenda ya kuandikwa Katiba bora ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pasitokee yeyote kudanganyika na kinachoitwa "maridhiano" maana kutafanya Katiba isipatikane muda mfupi ujao.

Kimsingi, Katiba mpya itaruhusu kuwepo kwa mazingira ya uchaguzi huru na wa haki, kukomaa kwa demokrasia, kuthaminiwa kwa haki na uhuru wa kila mwananchi.

***Mwandishi ni Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba Tanzania (Jukata).***



Habari

# Tajiri Afrika Kusini ashinda kesi uchimbaji graphite



Patrice Motsepe

Na Mwandishi WETU

MWEKEZAJI maarufu wa Afrika Kusini na mmoja wa matajiri wakubwa Afrika, Patrice Motsepe, amepata ushindi wa kisheria kwenye shauri la uchimbaji madini Tanzania.

Mahakama Kuu ya Johannesburg, Afrika Kusini wiki iliyopita ilitupilia mbali madai yaliyokuwa yamewasilishwa dhidi ya kampuni ya uwekezaji, African Rainbow Capital (ARC) inayomilikiwa na Motsepe katika mgogoro wa mradi wa kuchimba madini ya graphite nchini Tanzania.

Uamuzi huo unahusiana na kesi iliyofunguliwa katika mahakama za Tanzania na kampuni za Pula Group pamoja na Pula Graphite Partners Tanzania, ambazo zilidai kuwa ARC, kampuni dada ya African Rainbow Minerals (ARM), kampuni ya ARCH Sustainable Resources (ARCH) pamoja na Motsepe binafsi, zilikiuka makubaliano ya kutunza siri za kibiashara (Non-Disclosure Agreement – NDA) yaliyohusiana na mradi wa utafutaji wa graphite nchini Tanzania.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na ARC, Mahakama Kuu ya Johannesburg imebaini kuwa Pula haikuwa na msingi wa kisheria wa kufungua madai ya uvunjifu wa mkataba dhidi ya ARC katika kesi inayosikilizwa Tanzania.

Mahakama pia imeamua kuwa kampuni hiyo haikuwa na haki ya kudai fidia kutokana na leseni ya utafutaji wa madini ambayo baadaye ilisimamishwa na kurejeshwa kwa mamlaka husika.

Chanzo cha mgogoro huo ni madai ya Pula kwamba taarifa za siri ilizoshirikisha ARM kupitia makubaliano ya NDA, zilivujishwa kwa ARC au ARCH.

Kampuni hiyo ilidai kuwa taarifa hizo zilitumika kuiwezesha ARCH kuwekeza katika kampuni pinzani ya Evolution Energy, inayojihusisha na shughuli za uchimbaji wa graphite nchini Tanzania, jambo ambalo lilisababisha Pula kupoteza fursa ya kupata faida kutoka katika mradi wake.

Hata hivyo, wakati wa usikilizwaji wa shauri nchini Afrika Kusini, Pula ilikiri mbele ya mahakama kuwa ARC haikuwa sehemu ya makubaliano ya NDA, hivyo isingeweza kuwajibishwa kwa madai ya uvunjifu wa mkataba huo.

Aidha, ilikubali kuwa haikuwa na msingi wa kudai fidia kuhusiana na leseni ya utafutaji ambayo tayari ilikuwa imesalimishwa kwa mamlaka zingine.

Mahakama pia ilibaini kuwa licha ya Pula kudai kuwa ilikuwa bado inamiliki haki ya utafutaji wa madini ilipofungua kesi nchini Tanzania mwaka 2023, baadaye ilidhihirika kuwa leseni hiyo haikuweza kuongezwa muda wake na ililazimika kusalimishwa.

Kufuatia hali hiyo, kampuni mpya iitwayo Pula Carbon, iliyosajiliwa mwaka 2023, ilipewa leseni mpya ya kufanya shughuli za utafutaji katika maeneo hayohayo, ingawa kampuni hiyo haikuwa sehemu ya makubaliano ya NDA wala shauri lililofunguliwa.

Inaendelea Uk. 41

# Tusihadaike...

Inatoka Uk. 40

Kwa kuwa makubaliano ya NDA yalikuwa yanatawaliwa na sheria za Afrika Kusini, ARC iliomba Mahakama Kuu ya Johannesburg itoe tafsiri ya kisheria kuhusu iwapo madai yaliyowasilishwa Tanzania yalikuwa na msingi chini ya sheria za nchi hiyo.

Baada ya kutoa hukumu hiyo, Pula iliwasilisha ombi la kukata rufaa, lakini baadaye iliondoa ombi hilo kabla halijasikilizwa. Kwa mujibu wa ARC, hatua hiyo inaifanya hukumu ya Mahakama Kuu ya Johannesburg kuwa ya mwisho na inayofunga pande zote.

Athari kwa uwekezaji

Mzozo huu unaibua maswali muhimu kuhusu namna mikataba ya kimataifa ya uwekezaji inavyotekelezwa pale inapohusisha sheria za nchi tofauti na shughuli zinazofanyika Tanzania.

Hali hii imeikumba mikataba mingi ya uwekezaji nchini huku katika kesi nyingi zilizofunguliwa serikali ikibwagwa na kulazimika kulipa fidia ya mabilioni ya dola.

Pia kesi hii inaonyesha umuhimu wa kampuni zinazowekeza katika sekta ya madini kuhakikisha mikataba ya usiri, ubia na uwekezaji inaandaliwa kwa umakini ili kupunguza hatari ya migogoro ya muda mrefu ya kibiashara.

Sekta ya graphite imeendelea kuvutia wawekezaji kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya madini hayo duniani, hususan katika utengenezaji wa betri za magari ya umeme na mifumo ya kuhifadhi nishati.

Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye akiba kubwa ya graphite Afrika, hali inayofanya migogoro ya umiliki wa miradi na haki za utafutaji kuwa na uzito mkubwa kwa mustakabali wa uwekezaji katika sekta hiyo.



*Askari Polisi wakiendelea kuimarisha ulinzi katika maeneo ya Jijji la Dar es Salaam kama walivyokutwa na Kamera ya Pambazuko katika Barabara ya Kilwa juzi.*

## Nionavyo




# Uanaharakati siyo uhalifu katika demokrasia

Na Steven MMBOGO

MSINGI wa kwanza wa dola ya kidemokrasia siyo uchaguzi. Msingi wake ni uhuru wa mwananchi. Uchaguzi ni matokeo ya uhuru huo; siyo mbadala wake.

Ndiyo maana katika falsafa ya utawala bora, serikali haiji ili kuwapa wananchi haki zao, serikali huundwa ili kulinda haki ambazo wananchi tayari wanazo kwa asili yao kama binadamu.

Mwanafalsafa John Locke alisisitiza kuwa binadamu huzaliwa na haki za asili; uhai, uhuru na mali, na kwamba serikali hupewa mamlaka kwa ridhaa ya wananchi ili kulinda haki hizo.

Serikali inaposhindwa kuzilinda au kuanza kuzikandamiza, inapoteza uhalali wake wa kimaadili.

Na hapo ndipo mikakati kadhaa ya kuzidai haki hizo huibuka. Moja kati ya makundi ya watu wanaoshinikiza kudai haki hizo ni wanaharakati.

Hivyo basi, uanaharakati siyo zawadi ya dola. Ni namna ambayo wananchi hutumia haki zao za msingi kuhakikisha kuwa dola inabaki ndani ya mipaka ya sheria.

Katika dola inayofuata utawala wa sheria, Katiba ndiyo sheria mama, ambayo hutambua haki kama vile, uhuru wa kutoa maoni, uhuru wa kupata na kusambaza taarifa, uhuru wa kukusanyika kwa amani.

Nyingine ni uhuru wa kujiunga na vyama au asasi na haki ya kushiriki katika uongozi wa nchi. Haki hizi hazikuwekwa ili zipambwe kwenye vitabu vya sheria. Ziliwekwa ili zitumike.

Ndipo uanaharakati unapopata uhalali wake. Mwananchi anapozitumia haki hizi kwa amani, kwa mujibu wa sheria, na kwa maslahi ya umma, hafanyi uhalifu, bali anatimiza wajibu wake kama raia katika jamii ya kidemokrasia.

Inaendelea Uk. 43

# Tusihadaike...

Inatoka Uk. 42

**Sheria za Kimataifa**

Baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia, mataifa yalitambua kuwa ukimya wa wananchi mbele ya dhuluma unaweza kuwa hatari kwa ubinadamu.

Ndiyo maana ziliwekwa nyaraka za kimataifa zinazolinda haki za kiraia na kisiasa.

Miongoni mwa nyaraka hizo ni azimio la Kimataifa la Haki za Binadamu (Universal Declaration of Human Rights - 1948), linalotambua uhuru wa maoni, kujieleza, kukusanyika na kushiriki katika utawala wa nchi, mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (International Covenant on Civil and Political Rights - ICCPR), unaolinda haki za kujieleza, kukusanyika kwa amani na kuunda vyama.

Na nyingine ni Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (African Charter on Human and Peoples' Rights), unaotambua kuwa wananchi wana haki ya kushiriki katika uongozi wa nchi zao na kutetea haki zao kwa njia za amani.

Kwa hiyo, uanaharakati siyo dhana ya kisiasa ya nchi moja, ni sehemu ya mfumo wa kimataifa wa kulinda utu wa binadamu.

**Tofauti kati ya serikali na dola**

Makosa mengi ya kisiasa huanza pale serikali inapojiona kuwa sawa na dola.

Hata hivyo, katika sayansi ya siasa kuna tofauti kubwa kwa kuwa serikali ni ya muda na dola ni ya kudumu.

Aidha, serikali hubadilika kupitia uchaguzi, lakini dola huendelea kuwepo bila kujali nani anatawala. Kwa hiyo, kuikosoa serikali si sawa na kuishambulia dola.

Mwanaharakati anayepinga sera fulani au anayetaka mageuzi ya sheria hashambulii taifa, bali anashiriki katika mchakato wa kuliboresha taifa.

Kuchanganya dhana hizi mbili ni hatari kwa demokrasia, kwa sababu hujenga mazingira ambayo ukosoaji wa sera unatafsiriwa kuwa uadui dhidi ya nchi.

Kwa nini Tawala za Kiimla huligeuza neno "mwanaharakati" kuwa tusi, ugaidi, uchochezi nk?

Katika tawala za kidemokrasia, mwanaharakati huonekana kama mshirika wa maendeleo, lakini tawala za kiimla, huonekana kama adui.

Utawala wa kidemokrasia hutafuta uhalali kupitia ridhaa ya wananchi na utawala wa kiimla hutafuta uhalali kupitia hofu. Na hakuna kitu kinachovunja hofu kuliko mwananchi anayesema ukweli hadharani.

Ndiyo maana tawala nyingi zenye hulka za kiimla hutumia mbinu zinazofanana; kama vile kuweka lebo za kisiasa kwa wakosoaji, kuwahusisha wanaharakati na maadui wa taifa bila ushahidi, kutumia propaganda badala ya kujibu hoja, kutengeneza mazingira ambayo wananchi wanaogopa kuzungumza.

Lakini historia inaonyesha kuwa ukweli una tabia ya kuchelewa kushinda, si kushindwa.

Mwandishi wa makala haya ni mtafiti wa masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi



Habari

# JAB yatambua rasmi wakongwe

Na Mwandishi WETU

BODI ya Ithibati ya Waandishi wa Habari (JAB) imezindua utambuzi rasmi wa wanataaluma wakongwe wa tasnia hiyo.

Katika kutambua na kuthamini mchango wao, JAB imepitisha Mwongozo wa Ithibati ya Maisha, utakaowawezesha wakongwe kutambulika kitaaluma kwa kuzingatia uzoefu wao badala ya vigezo vya elimu pekee.

Uzinduzi huo ulifanyika mwishoni wa wiki wakati wa Maadhimisho ya Siku ya JAB yaliyofanyika katika Kijiji cha Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ndani ya Maonyesho ya 50 ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba) jijini Dar es Salaam.

Akizungumza kwa niaba ya Mwenyekiti wa JAB, Tildo Mhando, Mjumbe wa bodi hiyo Dkt. Egbert Mkoko, alisema mwongozo huo unawahusu waandishi waliokuwa na umri wa kuanzia miaka 50 na zaidi wakati Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya mwaka 2016 ilipoanza kutumika.

Pia, katika kipindi hicho, tayari waandishi hao walikuwa tayari wametoa mchango mkubwa katika maendeleo ya sekta ya habari.


Alisema wengi wa waandishi hao hawakupata nafasi ya kufikia kiwango cha diploma kutokana na mazingira ya wakati huo, lakini walijifunza kwa vitendo na kujenga uzoefu uliowafanya kuwa sehemu muhimu ya maendeleo ya vyombo vya habari na ujenzi wa taifa.

Dkt. Mkoko ameeleza kuwa hatua hiyo inalenga kuhifadhi historia ya taaluma ya uandishi wa habari, kuthamini mchango wa waandishi wa kizazi cha mwanzo na kuhakikisha maarifa pamoja na uzoefu wao vinaendelea kuwa sehemu ya urithi wa tasnia hiyo.

Bodi hiyo imepongeza ushirikiano unaoendelea kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo katika kuimarisha taaluma ya uandishi wa habari, huku ikisisitiza umuhimu wa kuzingatia maadili, weledi na uwajibikaji kwa wanahabari.

Kaimu Mkurugenzi wa JAB, Wakili Patrick Kipangula, alisema uzinduzi wa Mwongozo wa Ithibati ya Maisha unaonyesha dhamira ya bodi ya kuhakikisha pamoja na kusimamia viwango vya taaluma kupitia sheria, mchango wa waandishi wa habari wakongwe unaendelea kutambuliwa, kuheshimiwa na kuwa sehemu ya historia ya maendeleo ya sekta ya habari nchini.

## Biashara yazorota Kariakoo...




*Maduka ya wafanyabiashara Kariakoo yakiwa yamefungwa kufuatia tishio la kuwepo wa maandamano Siku ya Maadhimisho ya Sabasaba jijini Dar es Salaam hivi karibuni. (Picha na Pambazuko).*

# Mkonge waanza kuinuka

Na Mwandishi WETU

MKONGE ni moja ya mazao ambayo yaliitambulisha Tanzania kuwa muuzaji nje wa mazao ya kilimo tangu nchi ilipopata uhuru.

Ni moja ya mazao makubwa; kahawa, korosho na chai, ambayo yalikuwa yakisafirishwa nje na kuingiza fedha za kigeni.

Lakini baada ya zao hilo kutopewa kipaumbele, likaanza kufifia kiasi kuwa uzalishaji wake ulishuka mno.

Lakini hivi sasa mambo yamebadilika kwani baada ya mkazo kuwekwa kwenye zao hilo, uzalishaji wake umeanza kupanda.

Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa uzalishaji wa zao la mkonge umeongezeka kutoka tani 56,000 mwaka 2023 hadi kufikia tani zaidi ya 72,000 mwaka 2025.

Ofisa Masoko wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), Best Rukanda, ameyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam katika Viwanja vya Sabasaba wakati wa Maonyesho ya Jubilei ya Dhahabu ya miaka 50 ya Sabasaba 2026.

"Kwa sasa uzalishaji wa zao hili la mkonge umepanda, kwa takwimu za mwaka jana 2025 ulikuwa tani 72,000 na ushee wakati mauzo ya mkonge uliosafirishwa nje yalikuwa zaidi ya tani 35,000…"

"Wakati Tantrade ikisheherekea Jubilei yao ya miaka 50, nasi kama bodi ambayo ndio wasimamizi na waendelezaji wa zao la mkonge na sekta nzima kwa ujumla tunajivunia kuongeza uzalishaji na ajira rasmi na zisizo rasmi," amesema Rukanda.

Pamoja na mambo mengine, Rukanda amesema kupitia zao hilo vijana wameweza kijiajiri kutengeneza bidhaa bunifu kama mikoba, kununua singa kwa wakulima na kuziuza huku wengine wakipata fursa ya kufanya kazi katika viwanda vya kuchakata mkonge.

Kwa upande wa kilimo amesema wameweza kutengeneza ajira zisizo rasmi katika ukataji wa mkonge katika mashine, uchakataji wa mkonge na uanikaji.

Rukanda ametoa rai kwa wakulima wa zao hilo kuzingatia kanuni za kilimo bora cha mkonge ili waweze kupata mazao bora yatakayojiuza katika soko.

Amewashauri watu wenye nia ya kuingia katika kilimo cha mkonge kuwasiliana na TSB moja ili wapatiwe elimu kuhusisna na zao hilo.

"Wakulima wanapofanya uchakataji wa majani yao waweke umakini ili kuhakikisha ubora wa singa zilizozalishwa. Singa bora na safi inamuwezesha mkulima kupata bei nzuri sokoni," amesema Rukanda.

Ameeleza kuwa mkonge una faida kubwa kiuchumi ikiwa mkulima atapata elimu ya kutosha kuhusu kanuni na taratibu za ulimaji wake hivyo ametoa rai kwao kuchangamkia fursa hiyo.

"Jukumu la bodi hii ni kutoa elimu kuhusu kilimo bora cha mkonge, lakini pia kuwezesha upatikanaji wa fursa za uwekezaji katika zao la mkonge, wakulima waje tuwashauri," amesisitiza Rukanda.



Na Anti MSHAURI





# Kutunza wazazi ni uwekezaji, baraka

HABARI za leo msomaji wangu wa safu ya uhusiano. Karibu tuweze kupata maarifa kuhusu maisha.

Wiki hii nitazungumza umuhimu wa kutunza wazazi.

Kutunza wazazi ni zaidi ya wajibu. Ni kumbukumbu ya upendo, ni shule ya maadili, na ni kioo kinachoonyesha jamii yetu imefikia wapi katika utamaduni wetu wa Kitanzania ambapo wazazi wamekuwa nguzo ya familia na taifa zima.

Msingi wa kwanza ni shukrani. Wazazi ndio waliosimama usiku na mchana kutulisha, kutufundisha, kutulipa ada na kutufuta machozi wakati wa magumu.

Hawakuwa na ratiba ya malipo. Walifanya kwa moyo. Sasa zamu imefika kwetu kuwa mkono wao wa kushoto na kulia.

Kuwatelekeza wakati wao wa uzee ni kama kufuta historia yetu wenyewe.

Wazazi ni maktaba inayotembea, ndani yao kuna hekima ya miaka mingi ambayo hupati darasani wala mtandaoni.

Wakati wa kukaa nao, kuwasikiliza na kuwahudumia, tunapata funzo la uvumilivu, heshima na upendo usio na masharti.

Watoto wetu wakiona namna tunavyowatunza wazazi wetu, wanajifunza moja kwa moja kuwa kesho nao watatutunza.

Lakini pia ni nguvu ya kiroho na baraka, katika mila na dini nyingi, baraka ya mzazi ina uzito mkubwa.

Mtoto anayemtunza mzazi kwa dhati huwa na amani ndani ya moyo wake, jamii yenye kuwaheshimu wazee wake huwa na mshikamano na haina mapengo mengi ya kizazi.

Tunapowapuuza wazazi tunajenga kizazi kinachofikiri maisha ni kusahau ulikotoka.

Lakini changamoto zipo, maisha ya leo ni magumu. Wengine wanasema kazi na familia zetu zimetuzonga. Hapa ndipo tunapopimwa, kutunza mzazi hakumaanishi lazima umpe nyumba au pesa nyingi kila mwezi.

Mara nyingi anachohitaji ni muda wako, simu ya kumuuliza hali, kumpeleka hospitali, au kukaa naye dakika chache na kumchekesha. Huduma ndogo ndogo hizo ndio zinampa nguvu ya kuendelea.

Tukikosa kuwatunza leo, kesho tutalia bila msaada. Na kama taifa tukipuuza wazee wetu tunapoteza mizizi yetu, kwani taifa lisilo na heshima kwa wazee wake halina mwelekeo.

Kwa hiyo umuhimu wa kutunza wazazi haupimwi kwa kile tunachowapa, bali unapimwa kwa kile tunachokuwa sisi – kwa kuwa nao karibu kama binadamu.

Kuwakumbuka wazazi au wazee ni uwekezaji wa upendo ambao unarudi kwetu kwa njia ya baraka, hekima na amani ya familia.

Tukutane wiki ijayo .

***Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.***

# Zaiylissa ndani ya vazi la Bazin



MWANAMITINDO na msanii wa filamu nchini, Zaiylissa, ameendelea kubamba kupitia mitindo ya mavazi anayovaa.

Wiki iliyopita alizidi kuzua gumzo kwenye mitandao ya kijamii baada ya kupigilia vazi la Bazin.

Vazi hilo la Bazin, kitambaa chake kinaheshimika kwa ubora na mng'ao wake huku ikidariziwa kwa michoro ya maua na kufanya kila sehemu ya vazi hilo ionekane ya kitamaduni zaidi.

Kilichokamilisha muonekano huo wa Zaiylissa ni Gele (kitambaa cha kichwani) huku akitupia na hereni, mkufu, bangili, handbag na viatu vyenye visigino vyembamba vilichongoza kwa mbele.

# Tumia mchele, maziwa kung'arisha ngozi yako

MCHANGANYIKO wa mchele na maziwa husaidia kung'arisha, kulainisha na kuondoa seli zilizokufa kwenye ngozi.

Zingatia yafuatayo;

* Chukua mchele kidogo usafishe vizuri halafu upike bila kuweka mafuta, ukiiva kabisa saga kwenye brenda kisha weka kwenye chombo kisafi.

* Weka maziwa kiasi kulingana na wingi wa mchele wako, koroga hadi vishikane vizuri.

* Unaweza pia kuweka asali kijiko kimoja kwenye mchanganyiko huo, kisha paka usoni na uache hadi vikauke kabisa.

* Baada ya kukauka osha uso wako na ukaushe kwa kitambaa kisafi.

* Fanya hivyo kila siku jioni utaona matokeo mazuri zaidi.





# Ndoa ya Zuchu, Diamond 'gudubai'

**Na Mwandishi WETU**

MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Zuchu ametangaza uhusiano wake wa ndoa na Diamond Platnumz umevunjika na kwamba wako kwenye hatua ya talaka.

Zuchu ametangaza uamuzi huo jana Julai 12, 2026 kupitia ukurasa wake Instagram, huku akisema amefikia uamuzi huo kwa moyo mzito baada ya miaka sita ya kuwa pamoja na Diamond na sasa ameamua kujichagua mwenyewe. "Hello my GPG, mimi na aliyekuwa mwenzangu tumeachana na tuko kwenye hatua ya talaka,"ameandika Zuchu. Akaongeza kuwa anamtakia kila la kheri aliyekuwa mwenza wake pamoja na familia yake.

"Kwa sasa nahitaji muda wa kupona, kujitazama upya na kuelekeza nguvu zaidi kwenye afya na kazi zangu…"

"Rizki imeisha, Alhamdulillah. Tulijaribu lakini Allah ana mipango yake na sina budi kuikubali,"ameandika.

Uamuzi huo wa Zuchu umekuja siku moja baada ya mama yake, Diamond kufanya sherehe ya siku ya kuzaliwa huku Zuchu akiwa hajahudhuria.

# Ray C awashukia wanaomwita 'msanii wa zamani'


**Na Mwandishi WETU**

MSANII wa muziki kutoka Tanzania, Rehema Chalamila maarufu Ray C, ambaye kwa sasa anaishi nchini Ujerumani, ametoa onyo kwa baadhi ya watu wanaomwita msanii wa zamani.

Ray C ametoa onyo hilo kupita ukurasa wake wa Instagram akisema; "Biashara ya kuitana msanii wa zamani mnitue, na Remmy Ongala mtasema wa lini? Na King Kiki je? Na Bi Kidude?

"Semeni tu mlichelewa kuja mjini!!! Ndiyo nishajiamulia hivyo!"


Msanii huyo kwa sasa ana wimbo wake mpya uitwao "Ongeza" ambao aliutoa wiki chache zilizopita.




Na John Marwa



Kombe la Dunia



Lamine Yamal



Kylian Mbappe

# Nusu fainali hizi, tutazifuatilia

HATIMAYE kutoka mataifa 48, yamesalia manne pekee katika safari ya kumsaka mwali wa Mzunguko wa 23 wa Fainali za Kombe la Dunia 2026, linaloendelea Marekani, Canada na Mexico.

Ilikuwa safari ya michezo 104, ikiwa ni kwa mara ya kwanza mashindano hayo makubwa duniani kushirikisha nchi 48 tofauti na idadi ya awali ya mataifa 32.

Michezo miwili ya hatua ya nusu fainali inayakutanisha mataifa manne, matatu kutoka Bara la Ulaya; Ufaransa, Hispania na England huku moja pekee kutoka Amerika Kusini; mabingwa watetezi, Argentina.

Nusu fainali ya kwanza tutawashuhudia mabingwa wa kombe hilo 2018, Ufaransa, kwenye fainali zilizopigwa nchini Urusi - dhidi ya mabingwa wa 2010, Hispania. Hawa waliibuka washindi katika fainali za kihistoria zilizofanyika kwa mara ya kwanza barani Afrika, Afrika ya Kusini.

Mtanange huo wa nusu fainali ya kwanza, utapigwa katika Dimba la AT&T uliopo Mji wa Arlinton katika Jimbo la Texas nchini Marekan. Uwanja huo unabeba mashabiki 95,000, ambao watakuwa mashahidi kushuhudia nani kati ya Hispania ama Ufaransa atatinga fainali, hapo kesho majira ya saa 4 usiku.

Nusu fainali ya pili itarindima kwenye uwanja wa Marcedes Benz uliopo Jimbo la Atlanta Georgia Marekani. Uwanja huo una uwezo wa kubeba mashabiki 71,000, ambao mabingwa watetezi, Argentina wakimenyana na mahasimu wao timu ya taifa ya England amba oni mabingwa mara moja 1966. Mechi hiyo itapigwa Jumatano majira ya saa 4 usiku.

Swali gumu linalohitaji muda kupata majibu, je ni nani kutinga Fainali ya Kombe la Dunia mzunguko wa 23 kati ya mataifa hayo makubwa katika ulimwengu wa kandanda?



# Obrigado Samagoal!



Na John MARWA

MWANZONI mwa juma lililopita taarifa iliyotikisa anga la soka nchini Tanzania, kwa moshi ulioleta mgagasiko kwenye mioyo ya wahafidhina wa kandanda, ni waraka wa nahodha wa Timu ya Taifa ya Tanzania, Mbwana Ally Samatta, kutangaza kutandika dalunga.

Miaka 15 iliyopita Samatta aliitwa kwa mara ya kwanza katika timu ya taifa 'Taifa Stars,' lakini ni miaka kumi mtawalia amekuwa mchezaji kiongozi wa wajukuu na vitukuu wa Julius Kambarage Nyerere.

Hakika hakuna asiyejua wala kutambua umuhimu na alama kubwa ambayo Samatta ameichora katika maendeleo ya soka la nchi, na njaa aliyoipanda katika mioyo ya vijana wengi wa ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Baada ya uamuzi huo, vilio vimekuwa vingi kila kona, wengi wakiamini kuwa bado mchezaji bora wa muda wote katika ardhi hii ya Waswahili anahitajika kuendelea kutoa burudani hasa kuelekea fainali za kihistoria za Mataifa ya Afrika, Pamoja Afcon 2027, zitakazofanyika Afrika Mashariki; Tanzania, Kenya na Uganda, kwa mara ya kwanza.

Wengine wakiamini mambo makubwa aliyoyafanya Samatta ya kuhadithiwa vizazi na vizazi, hapaswi kustaafu soka kwa waraka aliochapisha mitandaoni, bali katika Dimba la Benjamin Mkapa akiwa anaiongoza Stars nyumbani.

Samatta siyo jina tu, bali alama ya mapinduzi ya soka la Tanzania, mchezaji bora Afrika kwa wachezaji wa ndani, Mtanzania wa kwanza kucheza Ligi Kuu ya England, Ligi ya Mabingwa Ulaya, Fainali ya Carabao Cup, na Mtanzania pekee kucheza katika Dimba la Wembley pale kwa Mfalme.

Siwashangai wanaoona bado Samatta anahitajika kuiongoza Stars, lakini tamaa ya wengi ikiwa ni kiu ya taifa ni kuthibitisha kuwa nchi imekosa kuwaandaa akina Samatta wengine ambao leo wangekuwa wanaisimulia kwa vitendo hadithi ya 'Samagoal' ambayo imekuwa tamu kuliko ya Sungura na Fisi.

"Obrigado Samagoal" Kwaheri Goat'

*GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS' ASSOCIATION